



**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

**HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO  
YA AMALI**

**MHE. LELA MUHAMED MUSSA (MBM)**

**KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA  
2023/2024**

**Mei, 2023**



## YALIYOMO

UTANGULIZI .....	1
MIRADI YA SEKTA YA ELIMU.....	3
MUUNDO WA PROGRAMU .....	3
UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023 .....	4
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI .....	5
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	8
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU.....	11
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu .....	11
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti .....	13
Huduma ya Sayansi na Teknolojia .....	16
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	17
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu .....	19
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI .....	21
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali .....	21
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima .....	24
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU .....	26
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia .....	26
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	29
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu .....	31
Huduma za Maktaba .....	33
Huduma ya Urajisi wa Elimu.....	34
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu .....	37
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha	41
Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli ...	44

PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI .....	47
Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla .....	47
Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti .....	48
Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba.....	52
MAPATO.....	53
MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/2024	
KATIKA MFUMO WA PROGRAMU .....	53
Vipaumbele vya Wizara .....	53
MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU .....	57
PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA	
MSINGI .....	57
PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI.....	58
PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU.....	59
Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu .....	59
Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti .....	60
Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia .....	60
Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu.....	61
Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu.....	62
PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA	
AMALI.....	63
Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali .....	63
Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima .....	63
PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU .....	65
Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia .....	65
Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu.....	66
Huduma ya Ukaguzi wa Elimu .....	67
Huduma za Maktaba .....	67
Huduma ya Urajisi wa Elimu.....	68
Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha	69
Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano	
(TEHAMA).....	70

Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli ...	71
PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI .....	72
Programu ndogo Uongozi Kiujumla.....	72
Programu ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti.....	73
Programu ndogo ya kuratibu shughuli za Elimu Pemba .....	73
MAKADIRIO YA MAPATO.....	74
JUMLA YA GHARAMA ZA WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI .....	74
SHUKURANI .....	75
KIAMBATISHO.....	77



# HOTUBA YA WAZIRI WA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2023/2024

## UTANGULIZI

- 1. Mheshimiwa Spika,** Kwanza kabisa, namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uhai, uzima na afya njema tukaweza kumaliza Mfungo wa Mwezi Mtukufu wa Ramadhani na kusherehekea Sikukuu ya Eid-Fitr kwa salama na amani. Aidha, nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kukutana tena katika kikao hiki cha kujadili hotuba hii ya makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali. Aidha, namuomba aniwezeshe kuiwasilisha kwa ufasaha mkubwa ili wajumbe wote wa baraza lako hili waifahamu vizuri na waweze kuijadili, kuichangia na kuipitisha kwa kauli moja
- 2. Mheshimiwa Spika,** Pili nimshukuru na kumpongeza kwa dhati Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi kwa kuipa kipaumbele sekta ya elimu kutokana na mchango mkubwa katika Maendeleo ya Kiuchumi, Kijamii na Kisiasa. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie umri mrefu na afya njema wenye busara, hikma na maarifa zaidi ili aendelee kutuongoza vizuri. Wizara pia inatoa pongezi na shukrani za dhati kwa Makamo wa kwanza wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Othman Masoud Othman na Makamo wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa utendaji wao mzuri.

- 3. Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa nimpongeze Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa jitihada zake na mashirikiano anayotupa katika Maendeleo ya Zanzibar na Tanzania kwa ujumla.
- 4. Mheshimiwa Spika,** Shukurani za dhati nizifikishe kwa Wajumbe wa Kamati ya Ustawi wa Jamii chini ya uongozi mahiri wa Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mohammed Ahmada Salum kwa ushauri na maelekezo ya kimaendeleo wanayotupatia katika kuimarisha sekta ya elimu. Aidha, niwashukuru wajumbe wote wa Baraza lako hili tukufu kwa umakini wao na michango yao wanayoitoa kwa maendeleo ya nchi yetu, nasema ahsanteni sana.
- 5. Mheshimiwa Spika,** Kipekee napenda kumshukuru na kumpongeza Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali Mheshimiwa Ali Abdulghulam Hussein kwa kujitolea kwake na kunipa mashirikiano mazuri katika kutekeleza majukumu ya Wizara hii. Pia niwashukuru watendaji wote wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali wakiwemo Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini wa Elimu Pemba, Wakurugenzi, Wakuu wa vitengo, Wajumbe wa Bodi mbali mbali za Elimu, Maafisa wa ngazi mbalimbali wa Wizara, bila kuzisahau Kamati zetu za skuli kwa mashirikiano yao makubwa katika kuleta maendeleo ya elimu. Aidha, shukurani ziwafikie walimu, wazazi, wanafunzi na wadau wote wa elimu wa ndani na nje ya nchi kwa ushiriki na michango yao katika kusaidia harakati za utoaji na upatikanaji wa huduma ya elimu iliyo bora. Mwenyezi Mungu awazidishie moyo wa imani na uzalendo kwa nchi yetu.

6. **Mheshimiwa Spika**, Mwisho nawashukuru sana watendaji wa Ofisi ya Rais Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao ambao umechangia katika kuimarisha huduma za elimu katika mwaka wa fedha 2022/2023. Nimatumaini yetu kuwa ushirikiano huo utaimarika zaidi katika kuimarisha upatikanaji wa huduma za elimu bora katika Taifa letu
7. **Mheshimiwa Spika**, Utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka wa fedha 2022/2023 umetokana na mikakati ya Serikali katika kuhakikisha upatikanaji wa fedha na kuimarisha mashirikiano na wadau wote wakiwemo wananchi na wahisani wa ndani na nje katika kuchangia utekelezaji wa miradi mbali mbali.
8. **Mheshimiwa Spika**, kabla ya kuelezea matarajio ya bajeti ya mwaka 2023/2024, nitawasilisha utekelezaji wa mpango wa elimu kwa Mwaka wa fedha wa 2022/2023.

### **MIRADI YA SEKTA YA ELIMU**

9. **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2022/2023, Wizara ilitekeleza kazi zake kupitia miradi mikuu mitatu kama ifuatayo: -
  - i) Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi
  - ii) Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
  - iii) Uimarishaji wa Elimu ya Amali

### **MUUNDO WA PROGRAMU**

10. **Mheshimiwa Spika**, Wizara imetekeleza mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kupitia programu sita zifuatazo: -

- i) Programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi
- ii) Programu ya Elimu ya Sekondari
- iii) Programu ya Elimu ya Juu
- iv) Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali
- v) Programu ya Ubora wa Elimu
- vi) Programu ya Uongozi na Utawala

## **UTEKELEZAJI WA MPANGO WA WIZARA KWA MWAKA 2022/2023**

- 11. Mheshimiwa Spika,** Sasa naomba kuwasilisha utekelezaji wa mpango wa elimu kwa mwaka wa fedha 2022/2023, kupitia Programu sita. Programu hizi zimezingatia malengo ya maendeleo ya elimu ya Kitaifa na Kimataifa ikiwemo Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2020 - 2050, Vipaumbele vya sekta, Ilani ya Chama cha Mapinduzi pamoja na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).
- 12. Mheshimiwa Spika,** Programu zote sita zilitengewa jumla ya TSh. 309,815,073,480/- katika mwaka wa fedha 2022/2023. Kati ya fedha hizo, TSh. 249,063,699,480/- ni kutoka SMZ na TSh. 60,751,374,000/- ni kutoka kwa wahisani kwa ajili ya kusaidia miradi ya maendeleo. Kwa upande wa fedha za Serikali; Jumla ya TSh. 36,974,499,000/- zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, TSh. 149,976,400,000/- kwa ajili ya Mishahara na TSh. 62,112,800,480/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Miongoni mwa wahisani waliochangia bajeti ya Maendeleo ni Benki ya Kiarabu kwa Maendeleo ya Afrika (BADEA), Benki ya Dunia, Global Partnership for Education (GPE), KOICA, SIDA – Sweden, Table for Two (TfT), Shirika la Good Neighbor la Korea, Milele Zanzibar Foundation, IMF, UNICEF na UNESCO.

- 13. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya fedha zilizopatikana kutoka kwa SMZ na wahisani hadi kufikia Aprili 2023 ni TSh. 244,455,276,301/- sawa na asilimia 79 ya makadirio. Kwa upande wa Serikali jumla ya TSh. 216,887,072,698/- sawa na asilimia 87 na TSh. 27,570,003,603/- za wahisani sawa na asilimia 45 zilipatikana. Jumla ya TSh. 178,201,957,033/- sawa na asilimia 119 za SMZ zilitumika kulipia mishahara ya wafanyakazi, TSh. 23,680,340,170/ sawa na asilimia 38 zimetumika kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 15,004,775,495/- sawa na asilimia 41 zilitumika katika kazi za maendeleo. Kwa Upande wa wahisani jumla ya TSh. 27,570,003,603/- sawa na asilimia 45 zilipatikana na kutumika katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.
- 14. Mheshimiwa Spika,** Utekelezaji halisi wa mpango wa elimu kwa mwaka 2022/2023 kwa kila Programu ni kama ifuatavyo:-

### **PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

- 15. Mheshimiwa Spika,** Jukumu kuu la Programu hii ni kutoa na kusimamia elimu ya maandalizi na msingi kwa watoto wote kuanzia umri wa miaka minne.
- 16. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya TSh. 91,562,332,082/- zilitengwa kwa ajili ya utekelezaji wa Programu hii kwa mwaka 2022/2023. Kati ya fedha hizo TSh. 70,602,619,082/- ni kwa ajili ya kazi za kawaida zikiwemo TSh. 58,212,840,454/- za Mishahara ya wafanyakazi, TSh. 12,389,778,628/- kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 20,959,713,000/- kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya TSh 94,157,699,774/- sawa na

asilimia 103 zilipatikana. Shughuli zilizotekelezwa kupitia fedha hizi ni kama ifuatavyo:-

- i Wizara imefanya uhamasishaji wa uandikishaji wa wanafunzi katika Mikoa yote mitano ya Unguja na Pemba. Jumla ya wanafunzi 108,242 wa maandalizi wakiwemo wanafunzi 18,748 wa Vituo vya TuTu, na wanafunzi 380,641 wa msingi wameandikishwa Skuli kwa mwaka 2023 Unguja na Pemba.
- ii Jumla ya wanafunzi 90,787 wakiwemo wanafunzi 69,186 wa ngazi ya elimu ya Maandalizi na wanafunzi 21,601 wa ngazi ya elimu ya Msingi kutoka skuli 36 za Msingi za Serikali Unguja na Pemba wameendelea kupatiwa huduma ya lische.
- iii Jumla ya walimu 22 wamepatiwa mafunzo ya ukufunzi (TOT) katika program ya kumpima mtoto katika kipindi cha mpito kutoka darasa la maandalizi au nyumbani na kuingia darasa la kwanza na kuweza kutoa mafunzo kwa walimu 500 wanaosomesha darasa la kwanza.
- iv Jumla ya walimu 782 wapya wa vituo vya TuTu na walimu 894 wa Maandalizi na Msingi hadi kufikia April 2023 wamepangiwa kazi katika skuli mbalimbali Unguja na Pemba.
- v Wizara imekamilisha ujenzi wa skuli 29 zikiwemo skuli 22 za maandalizi na skuli 7 za msingi zinazojumuisha skuli mbili za elimu mjumuisho Unguja na Pemba. Aidha, Ujenzi wa Skuli ya Msingi Mwembeladu unaendelea na umefikia asilimia 75. Pia Wizara imekamilisha ujenzi wa vyoo 525 (Unguja 281 na Pemba 244) kupitia mradi wa UVIKO 19 na misaada ya wahisani mbalimbali

wakiwemo UNICEF, GPE na Save the Children.

- vi Wizara imefanya ukarabati wa skuli 9 za msingi Unguja na Pemba zikiwemo skuli za Jang'ombe, Mkwajuni, Chaani, Kwamtipura, Uzini, Chambani, Piki, Ukutini na Sizini. Aidha, Ukarabati mkubwa wa madarasa 13, Ukumbi wa Mitihani, Chumba cha Kompyuta na Ofisi ya Mwalimu Mkuu unaendelea katika skuli ya Msingi Kizimkazi mkunguni.
- vii Ujenzi wa madarasa 38 mapya Unguja na Pemba umekamilika. Miongoni wa Skuli zilizofaidika ni Skuli ya Kilimahewa, Kijini, Pwani mchangani, Ngagu, Wambaa, na Kipange
- viii Jumla ya wanafunzi 37,062 wa ngazi ya elimu ya msingiwamepatiwa vikaliyo Unguja na Pemba

### **Matokeo ya Muda Mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi 53,333 wapya wameandikishwa kuanza darasa la kwanza kwa mwaka 2023 katika skuli za Serikali na Binafsi. Kati yao 27,063 ni wanaume na 26,270 ni wanawake. Kati ya wanafunzi walioandikishwa darasa la kwanza, Wanafunzi 45,818 sawa na asilimia 85.9 wamepitia elimu ya maandalizi. Jadweli namba 15 (c) linatoa ufafanuzi zaidi.
- ii Jumla ya wanafunzi 380,641 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya msingi kwa mwaka 2023 ambao ni sawa na asilimia 105.4. Kati yao, wanaume ni 191,976 sawa na asilimia 106.1 na wanawake ni 188,665 sawa na asilimia 104.6, Jadweli namba 14 linatoa ufafanuzi zaidi.

## PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI

**17. Mheshimiwa Spika,** Lengo la Programu hii ni kutoa na kusimamia ubora wa elimu ya sekondari. Kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023, jumla ya TSh. 114,043,865,078/- zilitengwa kutekeleza shughuli za programu hii. Kati ya fedha hizo TSh. 70,527,705,078/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, TSh. 60,581,120,456/- kwa ajili ya malipo ya mishahara ya wafanyakazi na TSh. 43,516,160,000/- kwa kazi za maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2023, jumla ya TSh. 100,363,584,922/- zilipatikana sawa na asilimia 88. Utekelezaji kwa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i Jumla ya wanafunzi 18,893 wamefaulu mtihani wa Kidato cha Nne uliofanyika Novemba 2022, kati ya wanafunzi 6,097 wataendelea na masomo ya Kidato cha Tano katika skuli mbalimbali za Serikali za Unguja na Pemba na wanafunzi 107 wataendelea kusoma fani mbalimbali kwa ngazi ya Stashahada.
- ii Vifaa vya maabara na kemikali kwa ajili ya Mitihani ya Taifa ya Kidato cha Nne mwaka 2022 vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli za sekondari 188 zenye madarasa ya kidato cha nne na skuli 17 zenye kidato cha sita Unguja na Pemba. Aidha vifaa kwa somo la uchoraji (Fine Art), masomo ya maarifa ya nyumbani (home economy) na somo la Kompyuta vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli husika kwa mahitaji ya mitihani ya kidato cha Nne 2022.
- iii Vifaa kwa ajili ya somo la michezo (Physical Education) vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli ya Haile selasie. Pia vifaa vya somo la Kompyuta na somo

- la Nutrition vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli husika kwa ajili ya mitihani ya kidato cha sita inayotarajiwa kufanyika mwezi wa Mei 2023.
- iv Vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa masomo ya ufundi katika fani za Umeme, Ujenzi, Makenika na Komyuta vimenunuliwa na kusambazwa katika skuli za Ufundi Mikunguni na Kengeja.
- v Jumla ya wanafunzi 3,699 wanaoishi dahalia wanaendelea kupatiwa huduma ya chakula Unguja na Pemba. Dahalia hizo ni Mazizini, Hasnuu Makame, Donge na Mikunguni kwa Unguja na kwa upande wa Pemba ni dahalia za Fidel Castro, CCK kiuyu, Chasasa, Utaani, Mohamed Pindua na Kengeja ufundi.
- vi Jumla ya wanafunzi 2,627 kati yao wanawake 1,329 na wanaume 1,298 kutoka skuli za Serikali na Binafsi wanatarajiwa kufanya mitihani ya kumaliza kidato cha sita iliyoanza tarehe 02/05/2023.
- vii Walimu 5 na wanafunzi 40 wameshiriki katika mafunzo ya TEHAMA kupitia udhamini wa Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (UCSAF) yaliyofanyika katika Chuo cha Dar es Salaam Institute of Technology (DIT) Tanzania Bara. Aidha, Jumla ya wanafunzi wanawake 61 wamepatiwa mafunzo ya CODE kupitia programu ya African Girls Can Code Initiative (AGCCI) inayodhaminiwa na UN-WOMEN kupitia ufadhili wa ubalozi wa Ubelgiji. Mafunzo hayo yalifanyika katika kituo cha ubunifu cha Jang'ombe.

- viii Jumla ya wanafunzi 162 wameshiriki katika kongamano la “Science Engeeniring Technolog and Mathematics” (STEM) lilofadhiliwa na Shirika la UNICEF.
- ix Wizara imekamilisha ujenzi wa Skuli 3 za Sekondari Unguja na Pemba katika maeneo ya Bwefum kwa Unguja na Makangale na Pujini kwa Pemba. Aidha, ujenzi wa Skuli za Mtopepo, Mfenesini, Gamba na Kifundi unaendelea.
- x Jumla ya wanafunzi 21,980 wa ngazi ya elimu ya sekondari wamepatiwa vikalio Unguja na Pemba
- xi Jumla ya Skuli 22 za Sekondari Unguja na Pemba zimefanyiwa ukarabati. Miongoni mwa Skuli hizo ni Skuli ya Haile Sellasie, Mikindani, Matemwe, Muanda, Mapinduzi, Ngwachani, Kiwani-Mauwani, Chasasa na Wete.
- xii Ujenzi wa Maabara 10 umekamilika katika skuli za Sekondari Tumbatu, Jendele, Fukuchani, Machui, Bumbwini kwa Unguja na kwa Pemba katika Skuli za Chambani, Uondwe, Shumba, Wambaa na Chanjamjawiri. Aidha, Wizara imekamilisha ujenzi wa dahalia mbili kwa ajili ya wanafunzi wa kike katika skuli ya Lumumba na Paje-Mtule.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi 104,025 wameandikishwa katika ngazi ya Elimu ya Sekondari ya awali (kidato 1–4). Kati yao, wanafunzi 50,449 wa kidato cha kwanza na pili wakiwemo wanaume 24,101 na wanawake 26,348.

Kidato cha tatu na nne kina jumla ya wanafunzi 53,576 wakiwemo wanaume 22,685 na wanawake 30,891. Jadweli Nam. 16 (b) linatoa ufafanuzi zaidi.

- ii) Jumla ya wanafunzi 6,512 wameandikishwa katika ngazi ya elimu ya Sekondari ya juu (kidato 5-6) wakiwemo wanaume 3,239 na wanawake 3,273. Kati yao wanafunzi 3,831 ni wa Kidato cha tano wakiwemo wanaume 1,898 na wanawake 1,933 na wanafunzi 2,681 wa kidato cha sita kati yao wanaume ni 1,341 na wanawake 1,340. Jadweli Nam.21 (a) linatoa ufafanuzi zaidi.

## **PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU**

- 18. Mheshimiwa Spika**, Madhumuni ya programu ya Elimu ya Juu ni kutoa elimu ya utaalumu itakayomuwezesha muhitimu kujiajiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja ambayo ni mafunzo ya ualimu na maeneo manne ya huduma, ikiwemo Huduma ya Ushauri na Utafiti; Huduma ya Sayansi na Teknolojia; Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu na Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo:-

### **Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu**

- 19. Mheshimiwa Spika**, Kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023 Programu hii ndogo ilitengewa jumla ya TSh. 1,309,592,203/- za SMZ kwa ajili ya kutoa mafunzo ya ualimu katika ngazi ya Stashahada na kutoa mafunzo ya ualimu kazini. Kati ya fedha hizo TSh. 517,833,821/- zilitengwa kwa matumizi mengineyo na TSh. 791,758,382/- kwa matumizi ya mshahara. Hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya TSh. 879,874,915/- sawa na asilimia 67%

zimepatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ndogo ni kama ifuatavyo:-

- i Wizara imeendelea kutoa mafunzo ya walimu kwa kufuatia programu za Stashahada ya msingi dini na kiarabu, Stashahada ya msingi sayansi, Stashahada ya msingi sayansijami, Stashahada ya sekondari dini na kiarabu, Stashahada ya sekondari (necta) na Astashahada ya maandalizi na msingi awali.
- ii Wizara kwa mashirikiano na Baraza la Mitihani la Tanzania (NECTA) imewapatia mafunzo washiriki 124 (Unguja 71 na Pemba 53) kuhusu mbinu bora za utungaji mitihani yenye vigezo na inayoendana na upimaji wa umahiri (Competence Based Assessment).
- iii Muongozo wa Mkufunzi na Kisaidizi cha Mwalimu imeandaliwa kwa lengo la kutayarisha muongozo wa kufundishia Mtaala unaozingatia umahiri kwa walimu wa Darasa la Saba Unguja na Pemba. Jumla Washauri 49 wa masomo wa kitaifa na kanda (Unguja 29 na Pemba 20) wamepatiwana mafunzo ya miongozo hiyo.
- iv Jumla ya skuli 30 za Sekondari Unguja (19) na Pemba (11) zilizofanya vibaya zaidi katika mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2021 zimefuatiliwa kwa kina kujua uwezo wa walimu juu ya uelewa wa maudhui ya masomo na mbinu za utungaji mitihani pamoja na kuwapatia mafunzo katika maeneo hayo. Baada ya ufuatiliaji huo kati ya skuli hizo 30, skuli 24 sawa na asilimia 80 ufaulu wao umeongezeka katika mtihani wa Kidato cha Nne mwaka 2022.

- v Jumla ya waajiriwa wapya 292 wa ualimu wamepatiwa mafunzo ya awali ya kada ya ualimu Unguja na Pemba (Pemba 194 na Unguja 98)
- vi Wizara imeimarisha mashirikiano na vyuo mbalimbali vya ndani na nje kwa lengo la kuimarisha mafunzo ya walimu. Miongoni mwa vyuo hivyo Chuo Kikuu cha Kiislamu cha Malaysia na IQBA (UNESCO). Mikutano mbalimbali na chuo hicho imefanyika kupitia mitandao na kuweza kubadilishana mawazo na kuamua maeneo ya mashirikiano katika taaluma ya ualimu.

### **Matokeo ya muda mfupi**

Jumla ya wanafunzi 847 wamehitimu mafunzo ya Ualimu kwa ngazi ya Astashahada na Stashahada ya Ualimu kwa mwaka 2022. Kati yao, wanafunzi 460 wakiwemo wanaume 39 na wanawake 421 ngazi ya Astashahada na wanafunzi 173 wakiwemo wanaume 40 na wanawake 133 ngazi ya Stashahada ni kutoka Chuo cha Kiislamu Mazizini Unguja. Wanafunzi 167 wakiwemo wanaume 47 na wanawake 120 ngazi ya Astashahada na wanafunzi 47 wakiwemo wanaume 16 na wanawake 31 ngazi ya Stashahada ni kutoka Chuo cha Kiislamu Kiuyu Pemba.

### **Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti**

20. **Mheshimiwa Spika**, Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti ina lengo la kuwaandaa wanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira. Huduma hii inatolewa katika Vyuo vikuu vitatu vilivyopo Zanzibar ambavyo ni Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Chuo cha Kumbukumbu ya Abdulrahman Al-Sumait na Chuo Kikuu cha Zanzibar

**21. Mheshimiwa Spika,** Jumla ya wanafunzi walioandikishwa katika vyuo vyote hivi vitatu imefikia wanafunzi 11,272 wakiwemo 6,730 wanawake na 4,542 wanaume. Kwa mwakawafedha 2022/23, Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) kilitengewa ruzuku ya TSh. 14,918,200,000/- kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Aidha Chuo kimekusanya jumla ya TSh. 14,041,111,019/- kutoka mapato ya ndani ya Chuo na kutumia TSh. 9,542,664,028/- kwa ajili ya maendeleo ya chuo. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 14,261,092,929/- sawa na asilimia 96 zimepatikana kutoka Serikalini. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya wafanyakazi wapya 10 wameajiriwa na kupangiwa kazi katika taasisi za chuo zikiwemo Skuli ya Kilimo, Skuli ya Biashara, Skuli ya Kompyuta, Mawasiliano na Taaluma za Habari, Skuli ya Afya na Sayansi za Tiba na Skuli ya Sayansi Asilia na Jamii.
- ii Chuo kinaendelea kuwalipia ada za masomo wafanyakazi wake 100 ambao wapo masomoni, kwenye ngazi mbali mbali za masomo zikiwemo Shahada ya Uzamivu (PhD) (47), Shahada ya Uzamili (37) na Shahada ya kwanza (15), Astashahada (1).
- iii Jumla wanafunzi wapya 3,079 wakiwemo wanaume 1,194 na wanawake 1,885 wamedahiliwa kujiunga na chuo kwa mwaka wa masomo 2022/2023 katika ngazi mbali mbali.
- iv Chuo kimeanzisha maabara ya ubunifu WASTEX Lab Tunguu pamoja na kufanya ununuzi wa vifaa vya

maabara hiyo vikiwemo kompyuta na vifaa vyengine vya TEHAMA.

- v Chuo cha SUZA kimeendelea na utoaji wa ushauri wa kitaalamu kwa taasisi mbali za Serikali na zisizo za kiserikali na kufanya tafiti mbali mbali kupitia ufadhili wa taasisi na mashirika mbali mbali ya ndani na nje ya nchi yakiwemo COSTECH, DANIDA, NORAD, UNICEF, UNDP, EU na Benki ya Dunia. Miongoni mwa taasisi zilizofanyiwa ni Wizara ya Afya, ZEMA, ZAFIRI, WEMA, UDSM na MUHAS.
- vi Chuo kimeingia makubaliano ya mashirikiano na kampuni ya New Wave Tech ya nchini Marekani na kuanza progamu za kukuza vipaji vya wanafunzi ambao wanajengewa uwezo kupata fursa za ajira katika makampuni na viwanda. Jumla ya wanafunzi 406 wanaendelea kunufaika kupitia mashirikino hayo.
- vii Matayarisho ya awali ya ujenzi wa majengo matatu katika kampasi ya Tunguu kupitia mradi wa HEET yameanza. Majengo yenyewe ni jengo la kituo cha maabara ya Sayansi Asilia, jengo la dakhalia za wanafunzi na jengo la maabara za Skuli ya Kilimo pamoja na ununuzi wa vifaaa vya Tehama kupitia mradi huo.

### **Matokeo ya muda Mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi 3,005 wamedahiliwa katika ngazi mbali mbali. Kati yao wanawake 1,168 na wanaume 1,837.

- ii Jumla ya wanafunzi 1,913 kati yao wanaume 752 na wanawake 1,161 wamehitimu katika ngazi za Shahada na Stashahada katika programu mbali mbali zikiwemo za Shahada ya Uzamivu, Shahada ya Uzamili, Shahada ya Kwanza, Stashahada na Astashahada na wanafunzi wote hawa wametunikiwa vyeti.

### **Huduma ya Sayansi na Teknolojia**

**22. Mheshimiwa Spika**, huduma ya Sayansi na Teknolojia ni miongoni mwa huduma muhimu katika kuinua kiwango cha Elimu ya Uhandisi, Sayansi na Teknolojia na kuimarisha maendeleo ya uchumi wa nchi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia. Kwa mwaka 2022/2023, Taasisi hii ilitengewa ruzuku ya TSh. 2,048,400,000/- Kati ya fedha hizo, TSh 519,200,000/- kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh 1,529,200,000/- kwa ajili ya mishahara. Hadi kufikia April 2023, Jumla ya Tsh 2,122,828,835/= za SMZ zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 104%. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya wanafunzi wapya 988 wamesajiliwa kati yao wanaume 850 na wanawake 138 kwa fani zote za Taasisi, Shahada ya kwanza 91 (30 wanawake na 61 wanaume), Stashahada 294 (90 wanawake na 204 wanaume), Astashahada ni 603 (18 wanawake na 585 wanaume).
- ii Jumla ya watumishi 6 (2 wanawake na 4 wanaume) wameajiriwa katika Taasisi kwenye kada ya ukufunzi.
- iii Wizara kupitia Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia imeanzisha programu mpya za mafunzo ya

Shahada ya kwanza ya uhandisi Telecommunication and network, Stashahada ya Digital Design and Development, usarifu wa mazao ya baharini na usarifu wa matunda na mboga mboga.

- iv Taasisi imeimarisha mashirikiano na Taasisi za ndani na nje ya nchi vikiwemo vyuo vya International Certificate in Digital Literacy (ICDL) Africa, IPB University (Indonesia), AP University Applied Science Belgium, Aksaray University (Turkey), Zanzibar Road Transport and Safety Authority (ZARTSA).

### **Matokeo ya muda Mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi 1,880 wakiwemo wanawake 298 na wanaume 1,582 wanaendelea na masomo katika fani mbali mbali zikiwemo, Shahada ya Uhandisi wa ndege, Stashahada ya Uhandisi Majenzi, Shahada ya Uhandisi Umeme na Elektroniki na Shahada ya Telecommunication and Network, Stashahada ya teknolojia ya habari mawasliano na biashara, Stashahada ya Usimamizi wa Maabara, pamoja na mafunzo ya Cheti cha Ufundi Stadi.

### **Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

- 23. **Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar inatekeleza majukumu makuu matatu, ambayo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wenye sifa za kujiunga na masomo ya elimu ya juu, kusimamia na kufuatilia nafasi za ufadhili wa masomo kutoka kwa washirika mbali mbali wa maendeleo nje na ndani ya Tanzania na kukusanya marejesho ya mikopo ya wanafunzi kutoka kwa wanufaika wote. Kwa mwaka wa fedha

2022/2023, jumla ya TZS 12,426,600,000 bilioni za ruzuku kutoka Serikalini zilitengwa kwa ajili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya na wanaoendelea na masomo ya Elimu ya Juu. Hadi kufikia April 2023, jumla ya TZS 7.96 bilioni sawa na asilimia 55 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya wanafunzi 4,875 wamepatiwa mikopo ya elimu ya juu wakiwemo wanafunzi wapya 1,815 na wanafunzi 3,060 wanaoendelea na masomo. Aidha, wanafunzi 4 wapya wamepatiwa nafasi za ufadhili wa masomo nje ya nchi kutoka Serikali ya Ufalme wa Ras al-Khaimah.
- ii Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeendelea na utaratibu wa kutoa ufadhili wa masomo ikiwa ni zawadi kwa wanafunzi bora waliofaulu vizuri zaidi kwa daraja la kwanza katika mitihani ya Taifa ya Kidato cha Sita katika masomo ya Sayansi, Biashara na Sanaa. Wanafunzi 157 wakiwemo wapya 30 na wanaoendelea na masomo 127 wamefaidika na utaratibu huu.
- iii Jumla ya wanafunzi wapya 61 wamepatiwa ufadhili wa masomo kwa vyuo vya ndani ya nchi wakiwemo 28 wa Chuo Kikuu cha Zanzibar kilichopo Tunguu kupitia ufadhili wa taasisi za Darul Iman. Aidha, wanafunzi 33 wa Chuo Kikuu cha Abdulrahman Al – Sumait cha Chukwani walipatiwa ufadhili kupitia Shirika la “Direct Aid” (African Muslim Agency).
- iv Jumla ya wanafunzi 1,284 wakiwemo wanafunzi 874 wanaosoma vyuo vya Zanzibar, 297 wa vyuo vya

Tanzania Bara na 113 wa vyuo vya nje ya Tanzania wanatarajiwa kuhitimu masomo yao katika fani na ngazi mbali mbali za elimu ya juu.

### **Matokeo ya muda Mfupi**

- i Jumla ya TSh. 2.9/- bilioni zimerejeshwa mpaka kufikia mwezi April 2023 sawa na asilimia 60 ikiwa ni marejesho ya mkopo ya TSh. 4.8/- bilioni ya lengo lililowekwa.
- ii Jumla ya wanafunzi 4,875 wanapokea mkopo wakiwemo 1,815 wapya na 3,060 wanaoendelea.

### **Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu**

**24. Mheshimiwa Spika**, huduma ya uratibu wa Elimu ya Juu ina jukumu la kusimamia na kutathmini maendeleo ya elimu ya juu na inatekelezwa na Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya Juu. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Kitengo kilitengewa jumla ya TSh. 50,000,000/= kutoka Serikalini. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 13,615,000/= sawa na asilimia 27.2 zimepatikana. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i Wizara kupitia Kitengo cha Uratibu wa Elimu ya juu kimefanya Maonesho ya tatu ya Wiki ya Elimu ya Juu ambapo jumla ya washiriki 32 walipata fursa ya kuonesha kazi zao na jumla ya wadau 18,094 walitembelea katika mabanda ya maonesho hayo. Maonesho hayo yanalenga kutoa Elimu na miongozo kwa wadau wote wa Elimu pamoja na wanafunzi wanaomaliza kidato cha sita ambao wanatarajiwa kujiunga na Elimu ya Juu ili waweze kuchagua fani za Vyuo Vikuu zinazoendana na masomo yao.

- ii Jumla ya programu nne za uhamasishaji juu ya kupunguza masuala ya udhalilishaji katika taasisi za elimu ya juu, skuli na jamii kwa ujumla zimefanyika.
- iii Nafasi za ufadhili wa masomo zimetangazwa kutoka kwa nchi wahisani 14 wakiwemo Algeria, Jumuiya ya Madola, Hungary, China, Morocco, Mauritius, Misri, Saudi Arabia, Serbia, Romania, Oman, Chevening-United Kingdom, Netherland, na Pan African. Nafasi hizo zilijumuisha fani mbalimbali zikiwemo; Udaktari, Uchumi, Ukandarasi, Uwalimu, Uuguzi na Sayansi ya Mazingira, Kilimo, Usimamizi wa Biashara na Utawala, Siasa na Uhusiano wa Kimataifa, Maendeleo ya Jamii, na Sayansi ya tehama kwa viwango vya Shahada ya Kwanza, ya Pili na ya Tatu. Jumla ya waombaji 150 kati yao wanaume 101 na wanawake 49 waliwasilisha maombi yao. Matokeo ya maombi haya yanatarajiwa kutolewa mwezi wa Agosti,2024.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi watano (wanaume 4 na mwanamke 1) wamehitimu masomo yao katika fani mbalimbali zikiwemo shahada ya kwanza ya Sanaa ya ualimu, teknolojia katika uhandisi, Sayansi ya tiba na Programu ya computer. Orodha ya wahitimu hao na fani zao za masomo zimewasilishwa Ofisi ya Rais, Katiba, sharia, Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- ii Jumla ya wanafunzi 150 wameomba nafasi za masomo nchini Morocco, Misri, China na Hungary. Majibu ya maombi yao yanatarajiwa kutoka mwezi Agosti 2023.

## **PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI**

**25. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwajengea vijana uwezo wa kupambana na soko la ajira kwa kuwapatia mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala. Programu hii ina programu ndogo mbili; Mafunzo ya Amali na Elimu Mbadala na Watu Wazima

### **Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali**

**26. Mheshimiwa Spika**, programu hii ndogo ilitengewa jumla ya ruzuku ya TSh. 9,634,300,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 7,690,100,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 1,944,200,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 4,371,189,893/= kutoka SMZ zilipatikana sawa na asilimia 45, Utekelezaji halisi kwa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imeandaa kipindi cha redio chenye lengo la kuzitangaza programu zinazotolewa kupitia Elimu ya Amali na kurushwa hewani kupitia kipindi cha Amka na ZBC katika ZBC TV. Aidha, makala maalumu inayoelezea “Mafunzo ya Kazi za Amali yanavyopunguza tatizo la Ajira kwa Vijana” imetolewa kupitia gazeti la Zanzibar Leo. Pia Mamlaka kwa kupitia ZBC redio na Televisheni imeweza kutoa matangazo mbalimbali kwa ajili ya usajili wa vijana katika vyuo vya Mafunzo ya Amali ambapo vijana 1,486 kati yao 739 ni wapya wamesajiliwa katika vyuo vitano vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa mwaka wa masomo 2023.

- ii Mamlaka imeweza kusimamia Mtihani wa Taifa wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali kwa vituo vya Serikali na binafsi. Jumla ya vituo 16 vimefanya mtihani wa Taifa wa Mamlaka ya Mafunzo ya Amali, vikiwemo vitano (5) vya Serikali na kumi na moja (11) vya Binafsi. Jumla ya wanafunzi 2329 walishiriki katika mitihani hiyo ambapo vijana 1,904 wamefaulu mitihani yao kwa mwaka 2022 sawa na asilimia 77 (wanawake 928 na wanaume 976).
- iii Jumla ya vituo 28 vinavyotoa Mafunzo ya Amali vimefanyiwa ukaguzi wa kawaida kwa lengo la kutathmini kiwango cha mafunzo yanayotolewa vikiwemo; Pama Culture, Hamasika Tailoring Center, Karume Vocatinal Training Center, Experience vocational Training, Zanzibar Commercial Training Center, Alnoor Vocational Training Center, Polisi Vocational Training Center, Modern Tailoring Training Center, Noah Training Center, Enlightenment Training Center, Chuo cha Mafunzo ya Amali Makunduchi, Chuo cha Mafunzo ya Amali Mwanakwerekwe, Makunduchi Vocational Training, kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo, Babel Training center, Zenth Training center na Dow Country Music Academy (DCMA), Juwalaza VTC, Vitongoji VTC na Zanzibar Mosquito Net
- iv Jumla ya vituo vitatu (3) vimepatiwa usajili mwaka 2022/2023, vituo viwili kwa upande wa Unguja na kimoja kwa Pemba navyo ni:- Al Asaah Vocational Training Center, Assalaam Vocational Training Center na Adult Vocational Training Center. Miongoni mwa

vituo hivyo, kituo kimoja (1) kimerudia usajili baada ya usajili wa awali kumaliza muda wake nacho ni Adult Vocational Training Centre.

- v Vifaa vya kufundishia na kujifunzia vimenunuliwa na kusambazwa katika vituo vya Mafunzo ya Amali Unguja na Pemba vikiwemo vifaa vya ufundi wa Aluminium, ushoni, mapambo, useremala, ufundi magari na mapishi.
- vi Mamlaka bado inaendelea kuratibu upatikanaji wa chakula kwa wanafunzi wanaoishi dakhalia ya Mkokotoni, Vitongoji, Daya na Makunduchi. Jumla ya wanafunzi 366 wa dakhalia hizo wakiwemo wanawake 143 na wanaume 223 wamepatiwa huduma hiyo kupitia michango ya Wazee wa wanafunzi.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya vijana wapya 739 (wanaume 443 na wanawake 296) wamejiunga na vyuo vya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali mwanzoni mwa mwaka 2023.
- ii Jumla ya TSh. 43,954,545/- zimerejeshwa na vikundi vya vijana vilivyopatiwa mkopo wa kuweza kujiajiri.
- iii Jumla ya vijana 495 wa vyuo vya Mwanakwerekwe, Mkokotoni na Vitongoji wamehitimu mafunzo yao. (Wanaume 281 na wanawake 214).
- iv Kuongezeka kwa vijana waliojiajiri kutoka vikundi 11 mwaka 2017 hadi kufikia vikundi 22 mwaka 2023.

## **Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima**

**27. Mheshimiwa Spika**, programu hii inatekelezwa na Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima na ina lengo la kupunguza kiwango cha wasiojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 34,436,735,317/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 587,833,822/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 598,901,495/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 1,037,618,930/- sawa na asilimia 3% zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya wanakisomo 5,508 wa Kisomo cha Watu Wazima wamefanyiwa Upimaji katika hatua zote nne za kisomo. Aidha wanakisomo 357 wa hatua ya nne wamekombolewa kupitia upimaji huo.
- ii Jumla ya wanafunzi 3,653 wakiwemo wanawake 987 na wanaume 2,666 wamesajiliwa kujiunga na madarasa ya Elimu Mbadala Unguja na Pemba. Kati yao 1,363 Unguja na 2,290 Pemba. Aidha, madarasa ya Elimu Mbadala yameongezeka kutoka 98 mwaka 2022, (Unguja 47 na Pemba 51) na kufikia 111, ongezeko hilo limetokana utekelezaji wa Programu ya kuwarejesha watoto skuli.
- iii Wizara imefanya maazimisho ya Juma la Elimu ya Watu Wazima. Uzinduzi wa Juma hilo ulifanyika Mkoa wa Kusini Unguja katika kijiji cha Paje, ambapo Wanakisomo wamepata fursa ya kujifunza upandaji wa mwani na kilele kilifanyika Mkoa wa Mjini

Magharibi katika Wilaya ya Mjini kwenye Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo.

- iv Jumla ya vikundi vya wanakisomo 58 (16 Unguja 42 Pemba) vyenye jumla ya wanachama 1,113 wakiwemo wanawake 1,013 na wanaume 100 vimeendelezwa kwa lengo la kuwapunguzia wanawake utegemezi na umasikini wa kipato.
- v Jumla ya wanafunzi 668 wakiwemo wanaume 358 na wanawake 310 wamesajiliwa katika vituo vya kujiendeleza kwa Unguja na Pemba. Aidha, wanafunzi 84 (wanawake 77 na wanaume 7) walioshindwa kuendelea na masomo yao baada ya mtihani wa Kidato cha Pili na cha Nne wameandikishwa katika Kituo cha Sayansi Kimu Forodhani kusomea fani ya Upishi, Ushoni, Kudarizi na Kufuma.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya wanakisomo waliomo madarasani ni 6,453 wakiwemo wanaume 782 na wanawake 5,671.
- ii Jumla ya wanafunzi 25,961 wenye umri kati ya miaka 7 hadi 14 walioacha au kutokuandikishwa kabisa skuli wamerejeshwa na wanaendelea na masomo. Kati yao Unguja 13,150 (4,647 wanawake na 8,503 wanaume), Pemba 12,811 (5,161 wanawake na 7,650 wanaume).
- iii Jumla ya wanafunzi 497 wenye umri kati ya miaka 15 hadi 22 wameandikishwa katika Kituo cha Elimu Mbadala Rahaleo Unguja na Kituo cha Wingwi Mtemani Pemba. Kati yao, wanaume 278

na wanawake 219 Vijana hawa wanasomea fani mbalimbali zikiwemo Umeme, Ushoni, Upishi, Udobi, Mafunzo ya Kompyuta, Uchoraji, Kilimo na Ufugaji, Utunzaji Nyumba pamoja na masomo ya kawaida ili kuwajengea uwezo wa kujua kusoma, kuandika na kuhesabu.

## **PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU**

**28. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina lengo la kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu. Programu hii ina jumla ya programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama ifuatavyo:-

### **Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia**

**29. Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na kuratibu upatikanaji wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu. Shughuli za utoaji wa huduma hii zinatekelezwa na Taasisi ya Elimu Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, Taasisi ilitengewa ruzuku yenye jumla ya TSh. 984,300,000/, kati ya fedha hizo, TSh. 511,600,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 472,700,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya TSh. 1,090,014,995 /= sawa na asilimia 111 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

i Mtaala mpya wa umahiri kwa ngazi ya elimu ya Maandalizi na Msingi umekamilika na umeaza kutumika rasmi katika skuli zote za Serikali na binafsi kwa madarasa ya Maandalizi mwaka wa kwanza, Darasa la kwanza, darasa la nne na darasa la saba.

- ii Vifaa vya kufundishia kwa ajili ya matumizi ya mtaala mpya vimechapishwa na kusambazwa katika skuli za Unguja na Pemba kwa ajili ya madarsa yaliyoanza matumizi ya mtaala mpya. Vifaa hivi vinajumuisha jumla ya mihutasari 20,898, viwango vya kujifunza 13,600 na miswada ya vitabu na viongozi vya mwalimu 11,593.
- iii Jumla ya walimu 8,936 wa skuli za Serikali na binafsi Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya wakiwemo; walimu 2,082 wa maandalizi, 2,297 wa darasa la kwanza, 2,545 wa darasa la nne na 2,012 wa darasa saba. Aidha, maafisa 132 wa Wizara ya Elimu wamepatiwa mafunzo hayo wakiwemo Wakaguzi, Maafisa wa Baraza la Mitihani na Washauri wa Masomo katika vituo vya walimu Unguja na Pemba.
- iv Wizara imetayarisha mfumo wa upimaji na tathmini kwa wanafunzi wa ngazi ya elimu ya Maandalizi na Msingi wakiwemo wenye mahitaji maalumu. Kwa mujibu wa mtaala mpya kutakuwa na upimaji wa utayari wa kujifunza kwa watoto wa maandalizi mwaka II na upimaji wa kimataifa wa stadi za msingi za kujifunza (kusoma, kuandika na kuhesabu) kwa wanafunzi wa darasa la pili. Pia, kutakuwa na tathmini ya uwezo wa matumizi ya lugha ya Kiingereza kwa wanafunzi wa darasa la nne. Aidha, upimaji wa maendeleo ya kujifunza kitaifa utafanyika Darasa la Tatu kwa kupima ujuzi wa kusoma, kuandika, kuhesabu ubunifu na maadili na Darasa la Saba kupima uwezo wa mwanafunzi utakaomuwezesha

kuingia kidato cha kwanza. Aina zote hizi za upimaji zitasimamiwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu na Taasisi ya Elimu.

- v Wizara imefanya uhamasishaji kwa jamii kuhusu mabadiliko ya mitaala kwa ngazi za elimu ya maandalizi na msingi, ambapo jumla ya makala nne zilitayarishwa na kurushwa kupitia TV, redio na magazeti zikiwemo redio jamii ya Mteгани FM, Tumbatu FM na Redio Nuru FM, makala mbili kupitia Gazeti la Zanzibar leo na moja kupitia kipindi cha maelezo baada ya habari ZBC Redio. Pia jumla ya mikutano 11 ilifanyika katika Wilaya zote za Unguja na Pemba kwa ajili ya kutoa uelewa kwa Serekali za mitaa, Masheha, Kamati za skuli, Asasi za Kiraia, na wanajamii kuhusu mtaala mpya. Kadhalika, Taasisi imetayarisha rasimu ya jarida maalumu kwa lengo la kuzidi kuhamasisha jamii kuifahamu Taasisi ya Elimu na kazi zake pamoja na utekelezaji wa mtaala mpya kwa ujumla.
- vi Jumla ya miswaada 28 ya vitabu vya wanafunzi na 28 ya viongozi vya walimu imeandikwa na kufanyiwa tathmini ya udhibiti ubora kwa matumizi ya skuli za maandalizi na msingi za Zanzibar

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i) Mtaala mpya wa elimu ya maandalizi na msingi umeanza kutumika katika skuli zote za Serikali na binafsi kwa madarasa ya maandalizi 1, Darasa la 1, Darasa la 4 na Darasa la 7.

- ii Vifaa mbali mbali vya mtaala mpya kwa madarasa ya maandalizi I, darasa I, darasa IV na darasa VII vimesambazwa katika skuli za Unguja na Pemba.
- iii Jumla ya walimu 8,936 wa skuli za Serikali na binafsi walipatiwa mafunzo ya matumizi ya mtaala mpya.

### **Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu**

**30. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utoaji wa elimu. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Baraza la Mitihani la Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, huduma ya Upimaji na Tathmini ilitengewa ruzuku ya TSh. 6,009,500,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 5,481,700,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 527,800,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. TSh 3,986,574,730/- sawa na asilimia 66 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma ya Upimaji na Tathmini ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya wanafunzi 58,052 wa Darasa la Nne wakiwemo wanaume 29,723 na wanawake 28,329 waliandikishwa kufanya Mtihani. Kati ya Wanafunzi hao ni 56,160 sawa na asilimia 96.74 (wanaume 28,360 na wanawake 27,800) ya watahiniwa wote ya walifaulu Mtihani.
- ii Wanafunzi waliofaulu mtihani wa kumaliza darasa la saba ni 21,241 sawa na asilimia 86.42 ambapo wanaume ni 10,671 sawa na asilimia 50.23 na wanawake 10,570 sawa na asilimia 49.79 ya watahiniwa wote waliofanya Mtihani huo. Aidha, wanafunzi 90 wamefaulu kuendelea na masomo yao

katika madarasa ya michepuo ikiwa sawa na asilimia 0.358.

- iii Kwa upande wa kidato cha pili wanafunzi 27,588 sawa na asilimia 85.7 wamefaulu mtihani huo na kuendelea na masomo ya kidato cha tatu wakiwemo wanaume 11,818 sawa na asilimia 36.71 na wanawake 17,770 sawa na asilimia 48.99.
- iv Jumla ya walimu wanafunzi 339 sawa na asilimia 90.45 wamefaulu mitihani ya Cheti cha Ualimu Maandalizi (ECD) ambapo wanaume 66 na wanawake 273. Aidha, jumla ya walimu wanafunzi 9 (6 wamaume na 3 wanawake wanatarajiwa kufanya Mitihani ya kumaliza masomo ya Stashahada ya Ualimu kwa ngazi ya Msingi na Sekondari katika Vyuo vya Kiislamu vya Unguja na Pemba, inatarajiwa kufanyika kuanzia tarehe 22–31 Mei, 2023.

### **Matokeo ya Muda Mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi 56,160 waliofaulu mtihani wa Darasa la Nne ikiwa ni sawa na asilimia 96.67 kati ya hao, wanaume ni 28,360 sawa na asilimia 50.50 na wanawake ni 27,800 sawa asilimia 49.50 ya watahiniwa wote.
- ii Wanafunzi waliofaulu mtihani wa kumaliza Darasa la saba ni 21,241 sawa na asilimia 86.42 ambapo wanaume ni 10,671 sawa na asilimia 50.23 na wanawake ni 10,570 sawa na asilimia 49.79 ya watahiniwa wote waliofanya mtihani huo. Aidha, wanafunzi 90 wamefaulu kuendelea na masomo yao katika madarasa ya michepuo ikiwa na asilimia 0.358.

- iii Kwa upande wa kidato cha pili Wanafunzi 27,588 sawa na asilimia 85.70 wamefaulu Mtihani huo na kuendelea na masomo ya Kidato cha Tatu wakiwemo wanaume 11,818 sawa na asilimia 36.71 na wanawake 15,770 sawa na asilimia 48.99.
- iv Wanafunzi 339 sawa na asilimia 90.45 wamefaulu mtihani wa Cheti cha Ualimu Maandalizi (ECD) ambapo wanaume ni 66 na wanawake ni 273.

### **Huduma ya Ukaguzi wa Elimu**

**31. Mheshimiwa Spika**, utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa kuhakikisha kuwa elimu inayotolewa inafuata sera, sheria, miongozo na taratibu zilizopo. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, huduma hii ilipangiwa jumla ya ruzuku ya TSh. 1,536,800,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 696,400,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 840,400,000/- ni malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili, 2023, jumla ya TSh. 1,739,625,001/- zilipatikana sawa na asilimia 113, kati ya fedha hizo TSh. 1,566,825,001/- zilitumika kwa kulipia mishahara na TSh 172,800,000/- zilitumika kwa shughuli za kawaida za ofisi. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya walimu 2,039 wamekaguliwa kati ya 2,800 sawa na asilimia 73 ya makadirio ya walimu waliopangwa kukaguliwa kwa mwaka 2022/2023 na kupewa ushauri kulingana na masomo wanayofundisha, ushauri huu umezingatia juu ya upimaji endelevu kwa wanafunzi na utoaji mrejesho

- kwa kazi za wanafunzi Pamoja na ukamilishaji wa mada katika mihutasari.
- ii Ofisi imeandaa rasimu ya muongozo wa ukaguzi ya Vyuo vya Ualimu kwa lengo la kufanya ukaguzi katika vyuo hivyo na kuleta ufanisi katika ufundishaji. Rasimu hii itaanza kutumika mwaka wa masomo wa 2024.
  - iii Jumla ya vitabu 1500 vya miundombinu ya skuli vimechapishwa sambamba na hilo Walimu wakuu na walimu wakuu wasaidizi 332, wa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo kuhusiana na miundo mbinu ya skuli.
  - iv Jumla ya wakaguzi 88 walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mfumo wa ukaguzi, hali hii itasaidia kutoa ripoti za ukaguzi kwa haraka.
  - v Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu ilifanya upimaji kwa wanafunzi 1,803 wa darasa la Pili katika skuli 95 za Unguja na Pemba. Kwa masomo ya Kiswahili na hesabati Matokeo ya upimaji huu unaonesha kuwa asilimia 55 wanahitaji msaada katika hatua za juu za usomaji pamoja na matendo ya hesabati.
  - vi Jumla ya wakaguzi 88 walipatiwa mafunzo juu ya matumizi ya mfumo wa ukaguzi.

### **Matokeo ya Muda Mfupi**

- i Jumla ya skuli 878 (640 za Serikali na 238 za Binafsi) kati ya 938 sawa na asilimia 94 ya makadirio ya skuli zilizopangwa kukaguliwa kwa mwaka 2022/2023 zimekaguliwa hadi kufikia mwezi wa Aprili, 2023.

Kati ya skuli hizo 85 ni za Maandalizi, 442 za Msingi na 319 za Sekondari.

- ii Jumla ya skuli 219 za Serikali zimekaguliwa mara mbili kati ya skuli 221 kwa mwaka 2022/2023 sawa na asilimia 99. Aidha, skuli 32 zimekaguliwa kwa ajili ya kupatiwa usajili.

## **Huduma za Maktaba**

**32. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu, nyaraka na nyenzo nyengine za taaluma kwa watoto, wanafunzi wa ngazi zote na jamii. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Bodi ya Huduma za Maktaba Zanzibar. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, huduma hii ilipangiwa kutumia ruzuku yenye jumla ya TSh. 904,900,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 463,500,000/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 441,400,000/- ni kwa malipo ya mishahara ya wafanyakazi. Hadi kufikia Aprili 2023, Jumla ya TSh. 742,234,940/= sawa na asilimia 82 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za huduma hii ni kama ifuatavyo:-

- i Jumla ya nakala 2,380 za magazeti zilinunuliwa. Aidha, jumla ya vitabu 7,706 vimeratibiwa na kupatiwa skuli na taasisi 31 za elimu za Zanzibar.
- ii Bodi ya Huduma za Maktaba imeendelea kuhamasisha wanafunzi na jamii juu matumizi ya maktaba kupitia vyombo vya habari na maonesho.
- iii Jumla ya watumiaji 44,333 walifika katika maktaba za Unguja na Pemba kwa kupata huduma mbali mbali wakiwemo watu wazima 22,016 (wanaume 12,610

na wanawake 9,406) na watoto 22,317 (wanaume 12,206 na wanawake 10,111). Huduma hizo ni pamoja na matumizi ya Mtandao (internet), uazimaji wa vitabu, usomaji na kutafuta taarifa.

- iv Bodi ya huduma za Maktaba imeendesha programu 33 za nje ya maktaba na 78 za watoto za ndani kwa wanafunzi kutoka skuli mbalimbali za serikali na binafsi.
- v Jumla ya maktaba tatu za Skuli zimeimarishwa kwa kupatiwa vitendea kazi vikiwemo vitabu, skuli zenyewe ni skuli ya Kidongo Chekundu msingi na Dimani kwa Unguja na skuli ya Jojo kwa Pemba.

### **Matokeo ya Muda Mfupi**

- i Jumla ya wanachama 967 wakiwemo wanaume 463 na wanawake 504 walisajiliwa katika Maktaba za Bodi.
- ii Idadi ya watumiaji wa maktaba imefikia 44,333 kati ya hao watu wazima ni 22,016 na watoto ni 22,371.

### **Huduma ya Urajisi wa Elimu**

**33. Mheshimiwa Spika,** huduma hii ina madhumuni ya kuhakikisha sheria, sera na taratibu za Wizara zinafuatwa katika skuli za Serikali na za binafsi. Huduma hii pia inatoa leseni kwa walimu na kuzisajili skuli za Serikali na za binafsi. Shughuli za huduma hii zinatekelezwa na Afisi ya Mrajisi wa Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, huduma hii ilipangiwa kutumia jumla ya ruzuku ya TSh. 248,000,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 129,600,000/- ni

kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 118,400,000/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 236,717,965/- sawa na asilimia 95 zimepatikana. Utekelezaji halisi wa huduma hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya kesi 44 za wanafunzi waliopata ujauzito (21 Unguja na 23 Pemba) zimeripotiwa katika afisi ya Mrajis na kwa kamanda wa polisi wa Mikoa husika. Kati ya kesi hizo, kesi 14 zimejadiliwa katika Afisi ya Mrajis Unguja na kesi 22 zimejadiliwa katika Afisi ya Mrajis Pemba.
- ii jumla ya kesi 31 za ubakaji na ulawiti wa wanafunzi (6 Unguja na 25 Pemba) zimeripotiwa katika ofisi ya mrajisi wa elimu na kufanyiwa kazi. Aidha, Jumla ya kesi 7 za ndoa za wanafunzi (3 Unguja na 4 Pemba) zimeripotiwa.
- iii Utoaji wa leseni mpya za walimu kwa kutumia mfumo wa kielektroniki unaendelea kwa walimu wa skuli za Maandalizi, Msingi na Sekondari wa Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja na Wete Pemba taarifa zao zimeshaingizwa katika kompyuta na kupigwa picha. Jumla ya walimu 1,382 (wanawake 874 na wanaume 508) Wilaya ya Kaskazini "A" Unguja na jumla ya walimu 1,154 (wanawake 681 na wanaume 473) Wilaya ya Wete Pemba wanatarajiwa kupatiwa leseni za kielektroni muda mfupi baada ya kukamilika.
- iv Jumla ya walimu 2,734 wakiwemo wa Cheti cha Ualimu, Stashahada, Shahada ya kwanza na ya pili walipatiwa leseni za kufundishia za muda wa miaka mitano. Aidha, Walimu 425 ambao hawajasomea

wamepatiwa leseni za kufundishia za muda wa mwaka mmoja. Walimu hawa wanashauriwa kujiunga na vyuo vya ualimu vilivyosajiliwa.

- v Jumla ya skuli 31 za Serikali zimepatiwa usajili ambapo (Unguja 8 na Pemba 23) Kati ya hizo Wilaya ya Chake Chake 7, Wilaya ya Micheweni 4, Wilaya ya Mkoani 3, Wilaya ya Wete 9, Wilaya ya kati 2, Wilaya ya Kusini 1, Wilaya ya Kaskazini “B”2, Wilaya ya Mjini 1, Wilaya ya Magharibi “A” 1 na Wilaya ya Magharibi “B” 1.
- vi Jumla ya skuli 51 za Binafsi zimewasilisha maombi ya usajili wa muda. Kati ya skuli hizo 36 za maandalizi, skuli 12 za msingi, skuli 2 za maandalizi, msingi na sekondari, skuli 1 ya sekondari. Kati ya hizo skuli 43 zimepatiwa usajili.
- vii Jumla ya vyuo 4 vya ualimu vimewasilisha maombi ya usajili wa fani ya ualimu ambapo vyuo 2 tayari vimekamilisha taratibu na kupatiwa usajili na vyuo vyengine viwili vinaendelea na taratibu za usajili, vikiwemo Chuo cha “Swahili Teacher College” kilichopo Kwarara Unguja, Chuo cha “Institute of Professional and Innovational Development” kilichopo chake chake Pemba, Chuo cha “Microtech Teacher College” tawi la Pemba na Chuo cha “Muslim Woman Teacher Centre” kilichopo chukwani Unguja.
- viii Jumla ya skuli 721 zilihakikiwa sawa na asilimia 60. Kati ya hizo; Unguja skuli 556 zikiwemo 88 za Serikali na 468 za Binafsi. kwa upande wa Pemba jumla ya skuli 165 zilihakikiwa kati ya hizo 99 za Serikali na 66 za Binafsi.

## **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya walimu 2,536 (1,382 Unguja na 1,154 Pemba) wakiwemo wanawake 1,555 na wanaume 981 Unguja na Pemba kupatiwa leseni zao za kielektroniki.
- ii Jumla ya skuli 43 za binafsi Unguja na Pemba zimepatiwa usajili wa muda. Aidha, Jumla ya skuli 31 za Serikali zimepatiwa usajili Unguja na Pemba.
- iii Jumla ya skuli 721 za ngazi mbali mbali za Serikali na Binafsi Unguja na Pemba zimehakikiwa.
- iv Jumla ya Vyuvo viwili vya ualimu vya binafsi vimesajiliwa kutoa mafunzo ya Ualimu. Vyuvo hivyo ni Chuo cha Swahili Teacher College kilichopo Kwarara Unguja na “Institute of Professional and Innovational Development” kilichopo chake chake Pemba.

## **Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu**

**34. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuifanya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano itumike katika ngazi ya utawala, kujifunza na kufundishia, kuimarisha huduma ya mawasiliano na kutunza usalama wa taarifa katika maisha ya kila siku. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 751,345,000/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 387,834,297/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 363,510,703/- ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023,

jumla ya TSh. 493,051,635/- zilipatikana ambazo ni sawa na asilimia 66 Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya watendaji 42 wa Ofisi kuu Mazizini wamepatiwa mafunzo ya mfumo wa e-office kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi.
- ii Jumla ya washiriki 86 wakiwemo maafisa wilaya, walimu wakuu wa wilaya ya kati na walimu wa sekondari na msingi wamepatiwa mafunzo ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji wao wa kazi na kuweza kuvitumia vifaa vya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia.
- iii Wizara imeimarisha miundombinu ya TEHAMA katika skuli mbali mbali Pamoja na unganishaji wa network katika ofisi za Wizara. Skuli zilizoungiwa network ni skuli ya Mahonda, skuli ya Biashara, skuli ya Hasnuu Makame, skuli ya Mh. Salum Turkey na skuli ya Mh. Mama Samia kwa Unguja na kwa Pemba ni Skuli ya Chasasa Sekondari, Dr. Ali Mohamed Shein Sekondari na Dr. Salim Ahmed Sekondari. Aidha, mfumo wa network ya jengo zima la Ofisi kuu ya Wizara Mazizini umewekwa upya na kufanyiwa backup ya server network.
- iv Wizara imefanya matengenezo ya vifaa mbalimbali vya TEHAMA vilivyo haribika katika Ofisi za Wizara na Skuli ili viweze kutumika inavyostahiki katika utendaji kazi. Vifaa vilivyofanyiwa matengenezo ni kompyuta 4 za idara ya sekondari, mashine 1 ya photocopy na kompyuta 3 za idara ya uajiri, kompyuta 2 za idara ya utumishi, mashine 1 ya photocopy na kompyuta

- 3 za Idara ya maandalizi na msingi, kompyuta 15 za skuli ya Biashara, kompyuta 7 na printer 1 za skuli ya Mahonda, printer 1 ya katibu wa waziri, printer 1 ya wahasibu, printer 1 ya ghala, mashine 1 ya photocopy ya idara ya TEHAMA, mashine 1 ya photocopy ya Kitengo cha Manunuzi na access point 2 zilizopo kwenye jengo kuu la Wizara.
- v Wizara kupitia KMEC imeandaa makala za vipindi 60 vya redio vya Stadi za maisha ambazo zina lengo la kuwasidia wanafunzi kukabiliana na changamoto mbali mbali ili watimize malengo yao, Makala za vipinchi hivi vinaendelea kurushwa hewani.
  - vi Kituo cha Habari za Elimu cha Kwarara KMEC kimeandaa vipindi 10 vya video vya kujifunza kiswahili kwa wageni na kurushwa hewani.
  - vii Wizara kupitia Kituo cha Habari za Elimu cha Kwarara (KMEC) imeandaa vipindi 40 vya happy Talk season 2 vimerikodiwa na vimekamilika kurekebishwa na vimehifadhiwa kwa ajili ya matumizi. Aidha, jumla ya makala 30 za vipindi vya redio vya Stadi za maisha ambazo zina lengo la kawasaidia wanafunzi kukabiliana na changamoto mbali mbali ili watimize malengo yao vinaendelea kurushwa hewani.
  - viii Kituo cha Habari za Elimu cha Kwarara (KMEC) kimeandaa matangazo ya kuhamasisha uandikishaji wa wanafunzi kwa mwaka 2023 ili kuwahamasisha wazazi na walezi juu ya umuhimu wa kuwapeleka watoto skuli.

- ix Wizara kwa Mashirikiano na Ofisi ya Mufti – Zanzibar kupitia KMEC wameandaa vipindi 15 vya Televisheni ambavyo vina lengo la kuwasaidia wanafunzi na walimu kujifunza mambo mbali mbali ya Dini ya Kiislam hasa kwa upande wa masomo ya dini na kiarabu kwa kuwasaidia wanafunzi darasani waweze kujibu vyema mitihani yao ya taifa.
- x Wizara kupitia KMEC inaendelea kuandaa na kurusha vipindi vya habari mbalimbali za kielimu na kijamii moja kwa moja (LIVE) katika chaneli yetu ya ELIMU FM RADIO. Miongoni mwa vipindi vinavyorushwa moja kwa moja (live) ni pembea, kutoka chumba chetu cha habari, E-morning, triangle, Ijumaa Munawar, Round sports na ladha muruwa lakini pia tunaendelea kurusha vipindi vilivyorekodiwa kama vile Happy Radio class, Happy Edu Quiz, Mwalimu wa wiki, na Kitabu chetu, lengo ni kuwasaidia wanafunzi katika kujifunza lakini pia kuwahabarisha wananchi.
- xi Wizara kwa mashirikiano na Shrika la kuhudumia watoto Ulimwenguni (UNICEF) wameandaa maonesho ya program za stadi za maisha kwa wanafunzi zinazojulikana kama KIJANAAMKA ambazo zina lengo la kuonesha changamoto wanazokabiliana nazo wanafunzi pamoja na suluhisho maonesho ya changamoto hizo.
- xii Wizara kupitia KMEC imeandaa programu 12 za chemsha bongo (Happy Edu Quiz) kwa wanafunzi wa skuli za sekondari za serikali na Binafsi, programu ambazo zimejikita katika masomo ya sayansi, Hesabu pamoja na Kiingereza lengo la programu

hizi ni kuwasaidia wanafunzi kuwa na kumbukumbu za muda mrefu za masomo yao ili waweze kufaulu katika mitihani yao ya taifa.

- xiii Idara ya TEHAMA kupitia KMEC imeandaa vipindi 50 vya happy radio class kwa masomo ya sayansi pamoja na Kiingereza kwa wanafunzi wa sekondari ambavyo vina lengo la kuchangia ufaulu wa wanafunzi wa sekondari kwa masomo ya sayansi.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya watendaji 42 wa ofisi kuu Mazizini wamepatiwa mafunzo ya mfumo wa e-office kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi.
- ii Jumla ya washiriki 86 wakiwemo maafisa wilaya, walimu wakuu wa wilaya ya kati na walimu wa sekondari na msingi wamepatiwa mafunzo ya TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji wao wa kazi na kuweza kuvitumia vifaa vya TEHAMA katika kufundishia na kujifunzia.

### **Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha**

- 35. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina jukumu la kuhakikisha upatikanaji wa elimu kwa watoto wote wakiwemo wenye mahitaji maalum, kutoa elimu ya stadi za maisha ikijumuisha ushauri na unasihi, jinsia, nidhamu endelevu, madawa ya kulevya na masuala yanayohusiana na afya ya uzazi. Programu hii inatekelezwa na Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha. Kwa mwaka wa fedha 2022/23 programu hii ilitengewa jumla ya TSh. 100,000,000/- kwa matumizi mengineyo. Hadi kufikia

Aprili, 2023, jumla ya TSh. 38,632,250/- sawa na asilimia 39 zilipatikana. Utekelezaji halisi wa shughuli za programu hii ndogo ni kama ifuatavyo: -

- i. Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kimefanya kongamano kwa wanafunzi ili kupata uwelewa juu ya Udhalilishaji na mimba za umri mdogo na ujauzito katika umri mdogo na athari zake na namna ya kujiepusha na vitendo hivyo. Jumla ya wanafunzi 116 (wanawake 63 na wanaume 53) na walimu 16 (wanawake 12 na wanaume 4) wa skuli 6 za msingi walishiriki kongamano hilo, skuli zenyewe ni: - Makadara, Jang'ombe A", Jang'ombe B", Kitogani, Muungoni na Ndiyani.
- ii. Jumla ya skuli 25 za msingi na sekondari zimefanyiwa ufuatiliaji ili kuangalia utekelezaji wa elimu mjumuisho na stadi za maisha pamoja na kukusanya data za wanafunzi wenye ulemavu ambao wamekusanywa kwa ajili ya kwenda kuendelea na masomo yao katika skuli mpya za elimu mjumuisho Jendele kwa Unguja na Pujini kwa Pemba. Aidha, Jumla ya wanafunzi 124 (wanawake 57 na wanaume 67) wenye ulemavu wa uoni na uziwi walianishwa kwa ajili ya kusajiliwa katika skuli hizo.
- iii. Jumla ya walimu 17 wa michezo Unguja na Pemba (wanawake 6 na wanaume 11) wamepatiwa mafunzo juu ya elimu ya afya ya uzazi kwa vijana. Lengo la mafunzo hayo ni kuwashajihisha walimu ili wapate uelewa wa namna bora ya kuhusisha mafunzo na michezo katika ufundishaji na ujifunzaji bora. Mafunzo hayo yameendeshwa kwa Mashirikiano na

Wizara ya Afya chini ya udhamini wa Shirika Engender Health ya Zanzibar.

- iv. Mafunzo juu ya Elimu ya Afya na lische yametolewa kwa walimu wakuu wa sekondari, maafisa wa elimu, walimu wa afya na mazingira Unguja na Pemba. Jumla ya washiriki 400 wakiwemo wanawake 338 na wanaume 62 Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo hayo.
- v. Mafunzo juu ya stadi za maisha yalitolewa kwa walimu na wanafunzi kwa lengo kujenga uwelewa juu ya stadi za maisha, jinsia, ushauri na unasihi, afya ya uzazi kwa watoto walio nje ya skuli. Skuli 17 (8 Unguja, 9 Pemba) zikiwemo 3 za sekondari na 14 za msingi zilihusika katika mafunzo hayo. Walimu 800 (wanawake 602 na wanaume 198) waliweza kupatiwa mafunzo. Aidha, Jumla ya wanafunzi 40,888 wakiwemo wanawake 23,246 na wanaume 17,642 walishiriki mafunzo hayo.
- vi. Mafunzo juu ya Elimu ya Afya na lische yalitolewa kwa walimu wakuu wa sekondari, maafisa wa elimu, walimu wa afya na mazingira. Jumla ya washiriki 438 wakiwemo wanawake 99 na wanaume 399 walishiriki mafunzo hayo Unguja na Pemba.
- vii. Jumla ya wadau 609; wakiwemo wajumbe wa kamati za skuli, wanafunzi wa sekondari, viongozi wa wizara ya Elimu na Mfunzo ya Amali, viongozi wa dini, wajumbe wa kamati ya ustawi wa jamii ya Baraza la wawakilishi, walimu wakuu na maafisa wa elimu walishiriki katika mikutano ya uhamasishaji kuhusu

elimu ya afya na lishe kwa kuwajengea uwezo juu ya ugawaji wa virutubishi vya madini chuma kwa wanafunzi waliofikia umri wa miaka 10-19 kwa sababu ya upungufu wa damu unaotokana na lishe duni na kupelekea ukosefu wa damu.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya wanafunzi 146 wamegundulikana na ulemavu wa uoni, akili na uziwi (84 Unguja na 62 Pemba).
- ii Jumla ya wanafunzi 40,888 (wanawake 23,246 na wanaume 17,642) walipatiwa mafunzo ya stadi za maisha mwaka 2022/2023. Mafunzo hayo yalifanyika katika skuli 17 zikiwemo 8 Unguja na 9 Pemba. Ukilinganisha na wanafunzi 23,074 (11,720 wanawake na 11,354 wanaume) waliofikiwa mwaka 2021/2022.
- iii Jumla ya walimu 438 (wanawake 99 na wanaume 399) walipatiwa mafunzo ya afya na lishe
- iv Jumla ya wadau 609 walihamasishwa juu ya ugawaji wa virutubishi vya madini chuma kwa wanafunzi waliofikia umri wa miaka 10-19 kwa sababu ya upungufu wa damu unaotokana na lishe duni.

### **Programu ndogo ya Michezo na Utamaduni katika Skuli**

**36. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mwanafunzi kimwili, kiafya na kiakili katika kujifunza kwa kupitia michezo. Shughuli za programu hii zinatekelezwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika elimu. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, programu hii

ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 793,405,508/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 547,833,822/- ni kwa matumizi mengineyo na TSh. 245,571,686/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 552,496,900/- sawa na asilimia 70 zilipatikana. Utekelezaji wa programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i Wizara imetoa mafunzo ya kuogelea kwa walimu na wanafunzi Unguja na Pemba ambapo jumla ya walimu 44 (28 Unguja na 16 Pemba) na wanafunzi 440 (280 Unguja na 160 Pemba) walipatiwa mafunzo hayo katika Skuli za Msingi na Sekondari. Aidha, walimu 220 ( 140 Unguja na 80 Pemba) walipatiwa mafunzo ya usalama na uokozi kwenye maji (Community education) Unguja na Pemba. Pia jumla ya walimu 24 (14 Unguja na 10 Pemba) walipatiwa mafunzo ya kufundisha kuogelea (Master trainers) Unguja na Pemba kwa skuli za Sekondari.
- ii Jumla ya walimu 20 wa Mchezo wa Cricket wamepatiwa mafunzo ya mchezo huo kwa mashirikiano na Chama cha Taifa kinachosimamia mchezo wa Kriket Zanzibar.
- iii Jumla ya wanafunzi 451 wa skuli za Msingi na Sekondari walishiriki katika mashindano ya Mbio za Nyika (Elimu Cross Country) yaliyoandaliwa na Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu.
- iv Wizara imeanza matayarisho ya kushiriki mashindano ya UMISSETA kwa Skuli za Sekondari na UMITASHUMTA kwa skuli za msingi yatakayofanyika mwezi June 2023 katika Mkoa wa Tabora. Jumla ya wanamichezo wanafunzi 189 wa Skuli za

Sekondari na 144 wa Skuli za Msingi Zanzibar wanatarajiwa kushiriki mashindano hayo. Michezo itakayoshindaniwa katika mashindano itajumuisha Mpira wa Miguu, Mpira wa Pete (Netball), Mpira wa Mikono (Handball), Mpira wa Meza, Riadha, Mpira wa Wavu na Mpira wa Kikapu.

- v Wizara ilifanya maadhimisho ya miaka 58 ya Elimu bila Malipo. Maadhimisho hayo yalijumuisha maonesho ya kitaaluma, makongamano ya michezo na uzinduzi wa miradi mbalimbali. Kilele cha Sherehe kilifanyika tarehe 23/09/2022 uwanja wa Amaani Unguja.
- vi Mashindano ya wanafunzi wa skuli za Msingi na Sekondari (Mapinduzi Cup) kwa fani ya Sanaa yamefanyika kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 59 ya Mapinduzi ambapo jumla ya skuli 30 kutoka Wilaya za Unguja zilishiriki.

### **Matokeo ya muda mfupi**

- i Jumla ya walimu 89 wamepatiwa mafunzo ya Michezo mbali mbali.
- ii Jumla ya skuli 11 zenye kufundisha Elimu ya Michezo (Physical Education) zimepatiwa vifaa vya Michezo.
- iii Jumla ya wanafunzi 343 wenye vipaji vya Michezo wanashiriki michezo mbali mbali katika ngazi ya Kitaifa.

## PROGRAMU YA SITA: UTAWALA NA UONGOZI

**37. Mheshimiwa Spika**, Programu ya Utawala na Uongozi ina lengo la kuhakikisha na kusimamia upatikanaji wa rasilimali bora katika utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya elimu. Programu hii ina programu ndogo tatu zikiwemo Programu ndogo ya Uongozi kwa ujumla, programu ndogo ya shughuli za Mipango, Sera na Utafiti na Programu ndogo ya uratibu wa shughuli za elimu Pemba.

### Programu ndogo ya Uongozi Kiujumla

**38. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kutoa ufanisi wa Uongozi na Utawala wa rasilimali za Wizara. Shughuli za programu hii ndogo zinatekelezwa na Idara ya Utumishi na Uendeshaji. Kwa mwaka wa fedha 2022/23, programu hii ilipangiwa jumla ya TSh. 8,995,727,943/- . Kati ya fedha hizo, TSh. 4,786,833,823/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 4,208,894,120/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 5,784,868,477/- zilipatikana sawa na asilimia 64. Utekelezaji wa kazi za programu hii ni kama ifuatavyo: -

- i Jumla ya wafanyakazi 300 (Pemba ni 117 na Unguja 183) walipata fursa ya kujiunga na masomo katika vyuo mbali mbali vya ndani na nje ya nchi katika ngazi tofauti baada ya kukamilisha masharti ya kiutumishi na ya vyuo.
- ii Jumla ya wafanyakazi 1,874 waliopewa likizo wamelipwa posho la likizo la Tshs 187,400,000. Aidha Wafanyakazi 340 wamelipwa malimbikizo yao ya mishahara ambapo jumla ya Tsh 148,425,047 zimelipwa kwa awamu tatu tofauti.

- iii Jumla ya wafanyakazi 1,820 wameajiriwa (909 kwa Unguja na 911 kwa Pemba). Aidha Wafanyakazi 187 walistaafu kazi kwa mujibu wa sheria, 95 kwa Unguja na 92 kwa Pemba. Pia Wafanyakazi 15 waliacha kazi kwa sababu mbalimbali. Aidha Wafanyakazi 14 walipewa uhamisho kwenda kuendelea na kazi katika Wizara na Taasisi mbali mbali, Wafanyakazi 19 wamechukua likizo bila ya malipo na wafanyakazi 31 wamefariki dunia, Mwenyezi Mungu awalaze mahali pema peponi Amiin.
- iv Katika kuendeleza juhudi za kuwasaidia wafanyakazi wetu katika kujikwamua na matatizo ya kimaisha, Wizara imewadhamini kupata mikopo ya Benki na Taasisi za kifedha zikiwemo Saccos, jumla ya wafanyakazi 596 Unguja na 321 Pemba walipata mikopo ya fedha taslim, vifaa vya ujenzi, vipando na vifaa vya matumizi ya nyumbani.

### **Matokeo ya muda mfupi**

Hadi kufikia mwezi wa April, 2023 Wizara ilikuwa na jumla ya wafanyakazi 18,520 kati yao 5,495 ni wanawake na 13,025 wanaume. Wafanyakazi 13,448 wapo Unguja na 5,054 wapo Pemba. Kati ya wafanyakazi wote hawa 15,153 ni wa kada ya ualimu na 3,349 ni wafanyakazi wasiokuwa wa kada ya ualimu.

### **Programu ndogo ya Mipango, Sera na Utafiti**

**39. Mheshimiwa Spika**, Madhumuni makubwa ya Programu hii ni kufanikisha na kuratibu utekelezaji wa Mipango, Sera na Utafiti ya Wizara. Programu hii ndogo inatekelezwa na Idara ya Mipango, Sera na Utafiti. Kwa mwaka wa fedha

2022/2023 programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TSh. 3,870,902,383/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 3,117,823,440/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 753,068,560/- ni kwa matumizi ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023 Jumla ya TSh. 1,282,040,377/- sawa na asilimia 33. zilipatikana. Utekelezaji halisi wa programu hii ni kama hivi ifuatavyo: -

- i Wizara inaendelea na utaratibu wa kuandaa Mpango Mkuu wa Elimu wa Miaka saba na (2023 -2030) utakaozingatia mapendekezo yatokanayo na ripoti ya Mageuzi ya sekta ya Elimu pamoja na malengo ya kitaifa na kimataifa. Mshauri elekezi kwa ajili ya kazi hii tayari ameshapatikana na itanza rasmi katikati ya mwezi Mei, 2023.
- ii Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mipango kazi ya Maendeleo ya Skuli za Sekondari umefanyika, jumla ya skuli 53 za Sekondari Unguja na Pemba zimefuatiliwa. Aidha jumla ya walimu 88 wa skuli za Msingi za Wilaya ya Kaskazini B na Wilaya ya Kati wamepatiwa mafunzo ya kuwasaidia kuaandaa mipango ya kazi ya Maendeleo ya skuli.
- iii Mkutano Mkuu wa Sita wa wadau wa elimu ikiwa ni miongoni mwa shughuli za ufuatiliaji na tathmini ya Sekta ya Elimu umefanyika ukiwa umebeba kaulimbiu ya “Kuufanyia kazi ushahidi kivitendo kuelekea mabadiliko ya mfumo wa elimu Zanzibar”. Jumla ya washiriki 150 walihudhuria mkutano huo wakiwemo walimu, wajumbe wa kamati za skuli, Maafisa wa elimu kutoka Wilaya zote za Unguja na Pemba, wanasiasa, taasisi zisizo za kiserikali, Jumuiya

za Kijamii, wahisani wa ndani na nje na viongozi mbalimbali kutoka sekta za Serikali.

- iv Wizara inaifanyia mapitio Sera ya Elimu ya Mwaka 2006 ili kuendana na mageuzi ya elimu na malengo mbalimbali ya kitaifa na kimataifa. Kazi itakamilika kabla ya mwisho wa mwezi Juni, 2023.
- v Utafiti wa SEACMEQ V unaotathmini ubora wa elimu ya msingi kwa wanafunzi wa darasa la sita katika masomo ya Lugha, Hesabati na Sayansi kwa sasa upo katika hatua ya uchambuzi wa data. Aidha, Utafiti wa kutathmini uwezo wa wanafunzi wa elimu ya msingi chini (lower primary) katika kujuwa kusoma, kuandika na kuhesabu unaendelea ambapo zoezi la kukusanya data limekamilika.
- vi Jumla ya madawati 4,032 ya wanafunzi wa ngazi ya elimu ya msingi yamenunuliwa na kusambazwa katika skuli mbalimbali za Serikali Unguja na Pemba. Aidha, Seti 17,425 za viti na meza zimesambazwa katika skuli za Sekondari Unguja na Pemba.
- vii Kitabu cha Takwimu za Elimu (Annual Statistical Abstract 2018 -2022) kimekamilika na tayari data zimewasilishwa kwa wadau mbali wa elimu wakiwemo maafisa elimu wa mikoa na wilaya, walimu na walimu wakuu wa skuli za serikali na binafsi, watakwimu wa mikoa na wilaya pamoja na maafisa mbali mbali wa Idara na Taasisi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.
- viii Zoezi la Sensa ya Mwaka ya Skuli (Annual School Census) limekamilika.

- ix Wizara imeimarisha mashirikiano na wahisani mbalimbali wa ndani na nje na kuweza kutiliana Saini mikataba ya miradi mbalimbali katika kuimarisha ubora wa elimu Zanzibar. Wahisani hao ni Benki ya Dunia kwa mradi wenye thamani ya Dola za Kimarekeani 50 mil wenye lengo la kuimarisha ubora wa elimu ya lazima, Benki ya Maendeleo ya Afrika (ADfB) kwa mradi wa thamani ya Dola za Kimarekeani 50 mil wenye lengo la kuimarisha ujuzi wa vijana katika soko la uchumi wa buluu.
- x Wizara imeandaa maandiko matatu ya miradi (Project Proposals) na kuiwasilisha kwa wahisani mbalimbali kwa kupata misaada. Maandiko hayo ya miradi inalenga kuimarisha na kuongeza idadi ya maabara za Sayansi katika skuli za Sekondari, Kuimarisha miundombinu ya Elimu na kuimarisha elimu ya ufundi Zanzibar. Miongoni mwa wahisani waliotumiwa maombi ya miradi hiyo ni OPEC Fund, Serikali ya Qatar na pia kuwasilishwa Serikalini kwa kutafutiwa wahisani.
- xi Wizara imeendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya elimu iliyokamilika na inayoendelea. Miongoni mwa miradi hiyo ni Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya lazima (ZIQUE), Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi na Mradi wa Uimarishaji wa Mafunzo ya Amali (SEBEP). Aidha Wizara imefuatilia utekelezaji wa programu mbalimbali zilizotekelezwa na fedha za Ahueni ya UVIKO 19.

## **Matokeo ya muda mfupi**

- i Ripoti za utekelezaji na tathmini ya maendeleo ya elimu zimeandaliwa.
- ii Jumla ya tafiti mbili zimefanywa uchambuzi wa data unaendelea.
- iii Jumla ya miradi mitatu mipya imekamilika na utekelezaji wake umeanza.
- iv Mashirikiano ya wahisani wa maendeleo katika sekta ya elimu yameimarika kwa kuongeza washirika wakiwemo Serikali ya Austria na Taasisi ya Teknolojia ya India (IIT madras).

## **Programu ndogo ya Uratibu shughuli za elimu Pemba**

**40. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ndogo ina madhumuni ya kuratibu na kusimamia shughuli zote za elimu kwa upande wa Pemba. Msimamizi Mkuu wa shughuli za programu hii ni Afisa Mdamini wa Elimu Pemba. Programu hii ndogo ilipangiwa jumla ya TSh. 4,135,467,967/-. Kati ya fedha hizo, TSh. 554,433,822/- ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na TSh. 3,581,034,145/- ni kwa malipo ya mishahara. Hadi kufikia Aprili 2023, jumla ya TSh. 1,268,598,680/= zilipatikana sawa na asilimia 31. Fedha za programu hii zilitumika katika kusimamia na kufuatilia shughuli zote na programu za elimu Pemba.

## MAPATO

- 41. Mheshimiwa Spika,** Wizara imeendelea kukusanya mapato kupitia usajili wa Skuli za binafsi, malipo ya leseni za walimu, ada za usajili wa skuli, ada za kiingilio kwa wanafunzi wanaojiunga na kidato cha sita. Hadi kufikia Aprili 2023, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imekusanya jumla ya TSh. 274,487,140.99/= kati ya TSh. 369,369,000/= zilizopangwa kukusanywa. Hii ni sawa ya asilimia 74.3 ya makadirio. Kati ya mapato yaliyokusanywa TSh. 128,174,868.62/= zikiwemo TSh. 114,485,869.62/= Unguja na TSh. 13,688,999.00/= Pemba zinatokana na malipo ya leseni za walimu na TSh. 146,312,272.37/= zikiwemo TSh. 134,678,232.47/= kwa Unguja na TSh. 11,634,039.90/= Pemba ni za usajili wa skuli za binafsi. hivyo Jumla ya TSh. 249,164,102.09/= zimekusanywa kwa Unguja na TSh. 25,323,038.90/= zimekusanywa Pemba.

## MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2023/2024 KATIKA MFUMO WA PROGRAMU

- 42. Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2022/23 naomba sasa niwasilishe Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mwaka wa fedha 2023/2024 kwa kuanzia na vipaumbele vya Wizara.

### Vipaumbele vya Wizara

- 43. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali imelenga kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya Elimu kwa kutekeleza vipaumbele 11 vifuatavyo: -

- i. Kuongeza uandikishaji na ufaulu wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu pamoja kuongeza asilimia ya watu wanaojua kusoma na kuandika kutoka asilimia 87.3 mpaka kufikia asilimia 90 mwaka 2025 na kuongeza idadi ya wanakisomo. Aidha, Wizara itaendelea kuzipatia skuli 42 za msingi zenye mazingira magumu huduma ya chakula na kuzipatia uji skuli zote za maandalizi za Serikali.
- ii. Kuandaa mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Elimu wa miaka 7 kuanzia mwaka 2023 hadi 2030 na kukamilisha Sera na Sheria ya Elimu zitakazoendana na mahitaji ya malengo ya taifa ili kukidhi ushindani wa soko la ajira wa ndani na nje ya nchi.
- iii. Kuimarisha Miundombinu ya elimu kwa kujenga madarasa 1000 ya Maandalizi, Msingi na Sekondari kupitia ujenzi wa skuli 31 za ghorofa, kujenga ofisi za Wizara Unguja na Pemba na ofisi tano za elimu za Wilaya zitakazojumuisha Maktaba na ofisi za wakaguzi wa elimu. Aidha Wizara itakamilisha ujenzi wa skuli mbili za Mtopepo na Muembeladu na kuzifanyia ukarabati mkubwa na mdogo skuli 21 Unguja na Pemba.
- iv. Kujenga vyuo vitano vya mafunzo ya amali; vitatu Unguja katika maeneo ya Jendele, Pangatupu na Bweleo na viwili Pemba katika maeneo ya Chambani na Tumbe kupitia mradi wa SEBEP (Skills Development for Youth Employability in the Blue Economy). Aidha, Mradi huu pia utajenga Chuo cha Ubaharia katika eneo la SUZA kampasi ya Nkurumah, utanuzi wa jengo la karakana ya makenikia katika eneo la Taasisi

ya Karume ya Sayansi na Teknolojia.

- v. Kuimarisha upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia katika ngazi zote za elimu, vikiwemo vitabu, kompyuta, vifaa vya wanafunzi wenye mahitaji maalum, miongozo ya walimu, samani mabuku na chaki. Aidha, Kuimarisha mafunzo ya amali kwa kuvipatia vyuo vya amali vifaa mbalimbali vya kujifunzia.
- vi. Kuimarisha huduma za dakhalia kwa kujenga skuli 3 za dakhalia, Kujenga dakhalia 4 katika skuli za Lumumba, Paje Mtule, Utaani na Chwakatumbwe pamoja na kuzipatia dakhalia usafiri wa magari.
- vii. Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika elimu kwa kuzipatia skuli vifaa vya TEHAMA na kuziunganisha na Mkonga wa Taifa.
- viii. Kuimarisha ukaguzi wa elimu kwa kuongeza idadi ya skuli na walimu waliokaguliwa pamoja na kuimarisha upimaji wa wanafunzi katika ngazi zote za elimu.
- ix. Kufungua tawi la chuo cha Teknolojia cha Nchini India “Indian Institute of Technology – IIT” kitakachoimarisha wataalamu wa fani za TEHAMA vZanzibar na ukanda mzima wa Afrika ya Mashariki. Aidha, kufanya ukarabati maabara za Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kwa mashirikiano na wahisani kutoka AUSTRIA.
- x. Kuajiri wafanyakazi 5,554 wakiwemo walimu na wafanyakazi wa fani mbalimbali. Pia kuwapatia walimu mafunzo juu ya matumizi ya mitaala mipya na kuimarisha mbinu na ufanisi wa ufundishaji wa

masomo ya Sayansi na Hisabati.

- xi. Kuendelea kuwapatia wanafunzi mikopo ya elimu ya juu kutoka wanafunzi 4,875 Mwaka 2023 na kufikia wanafunzi 6,060 mwaka 2024.

**44. Mheshimiwa Spika**, sasa naomba kuwasilisha mpango wa maendeleo ya elimu kwa mwaka wa fedha 2023/2024 kwa mfumo wa programu kama ifuatavyo:

**45. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali itaendelea kutekeleza malengo yake yaliyozingatia malengo ya Taifa ya Dira 2050, Ilani ya Chama cha Mapinduzi, Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDG), Mapendekezo ya ripoti ya mageuzi ya Sekta ya Elimu Zanzibar, Ahadi za Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na mikakati mengine ya kitaifa na kimataifa yenye lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya elimu nchini. Wizara pia, itaendelea kushirikiana na sekta nyengine zinazotoa huduma za jamii na kuimarisha uchumi ikiwemo Wizara ya Afya, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Maji na Nishati, Idara maalum za Serikali ya mapinduzi ya Zanzibar. Aidha Wizara itaendeleza mashirikiano na washirika wa maendeleo wa ndani na nje na mashirika yasiyo ya kiserikali na wananchi kwa ujumla katika utekelezaji wa mpango wake kupitia programu sita na miradi mbali mbali ya maendeleo ya elimu.

**46. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2023/2024, Wizara itatekeleza miradi mitano ya maendeleo ambayo ni:-

- i. Mradi wa Uimarishaji miundombinu katika elimu
- ii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi na Msingi
- iii. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Lazima
- iv. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Amali
- v. Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu

## **MAELEZO YA PROGRAMU ZA ELIMU**

47. **Mheshimiwa Spika**, yafuatayo ni maelezo ya programu za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali yanayohusisha Madhumuni, Matokeo ya muda mfupi, Viashiria na Shabaha za utekelezaji kwa kila programu.

### **PROGRAMU YA KWANZA: ELIMU YA MAANDALIZI NA MSINGI**

48. **Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kumuandaa mtoto kimwili na kiakili kwa ajili ya kupata elimu ya maandalizi na msingi na kumuwezesha kujua kusoma, kuandika na kuhesabu na kumtayarisha kwa elimu ya sekondari.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Wanafunzi waweze kujua kusoma, kuandika na kuhesabu

#### **Viashiria vya matokeo;**

- Asilimia ya uandikishaji.
- Uwiano wa idadi ya walimu kwa wanafunzi.
- Uwiano wa wanafunzi kwa darasa.

#### **Shabaha ya Utekekezaji;**

- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi

wa maandalizi kutoka asilimia 91.5 kwa mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 100 ifikapo mwaka 2024.

- Kuongeza kiwango halisi cha uandikishaji wanafunzi wa msingi kutoka asilimia 105.3 kwa mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 110 ifikapo mwaka 2024.

### **Gharama za Programu:**

Jumla ya TSh. 132,497,057,000/- zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 96,142,179,000/- ni kwa kazi za kawaida zikiwemo TSh. 85,494,093,000/- za mishahara ya wafanyakazi, TSh. 10,648,086,000/- kwa matumizi mengineyo na TSh. 36,354,878,000/- kwa kazi za maendeleo.

### **PROGRAMU YA PILI: ELIMU YA SEKONDARI**

- 49. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Elimu ya Sekondari madhumuni yake makubwa ni kumtayarisha mwanafunzi aweze kuendelea na masomo katika ngazi za juu zaidi.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Kutoa Elimu ya Sekondari.

#### **Viashiria vya matokeo;**

- Asilimia ya uandikishaji.
- Asilimia ya wanafunzi wanaomaliza elimu ya lazima.
- Uwiano wa idadi ya wanafunzi na walimu.
- Uwiano wa wanafunzi kwa madarasa.

#### **Shabaha za utekelezaji;**

- Kuongezeka kiwango cha uandikishaji wanafunzi wa sekondari ya awali (Kidato cha 1 – 4) kutoka asilimia 59 mwaka 2023 hadi kufikia asilimia 61 mwaka 2024.

**Gharama za Programu:**

Jumla ya TSh. 189,972,112,000/- zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 106,720,494,000/- ni kwa kazi za kawaida zikiwemo TSh. 93,089,044,000/- za mishahara ya wafanyakazi, TSh. 13,631,450,000/- kwa matumizi mengineyo na TSh. 83,251,618,000/- kwa kazi za maendeleo.

**PROGRAMU YA TATU: ELIMU YA JUU**

**50. Mheshimiwa Spika**, programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu itakayomuwezesha muhitimu kujijiri au kuajiriwa. Programu hii ina programu ndogo moja na maeneo madogo manne ambayo ni:

**Programu ndogo ya Mafunzo ya Ualimu**

**51. Mheshimiwa Spika**, programu hii ina madhumuni ya kuwawezesha walimu kuwa wabunifu, wataalamu na wenye uwezo wa kuongoza ili kukuza ubora wa elimu.

**Matokeo ya muda mfupi;**

- Uwepo wa walimu wenye umahiri watakaokuza ubora wa elimu.

**Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi waliohitimu mafunzo ya ualimu.
- Idadi ya programu za mafunzo ya Ualimu.

**Shabaha za Utekelezaji;**

- Kuongeza kiwango cha asilimia ya walimu wenye sifa kutoka asilimia 90.45 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 100 mwaka 2023.
- Kuongeza programu za mafunzo ya ualimu kutoka programu 6 za mafunzo tarajali (pre- service training)

mwaka 2023 hadi kufikia programu 10 mwaka 2024.

### **Huduma ya Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti**

**52. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kumtayarisha mwanafunzi kuingia katika fani za kitaalamu na ajira.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Ongezeko la wahitimu wa kiwango cha elimu ya Stashahada, Shahada ya kwanza, Shahada ya pili na Shahada ya tatu katika fani mbalimbali za kitaalamu zinazohitajika katika maendeleo ya nchi.

#### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Astashahada na Shahada, Shahada ya kwanza ya Uzamili na Uzamivu.
- Idadi ya Programu mpya zinazoanzishwa. Shabaha za Utekelezaji;
- Kuongeza idadi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu kutoka 11,272 mwaka 2023 hadi kufikia 12,400 mwaka 2024.
- Kuongeza idadi ya wanafunzi wanaomaliza ngazi ya Astashahada na Shahada, Shahada ya kwanza ya Uzamili na Uzamivu kwa mwaka kutoka 1,913 mwaka 2022/2023 kufikia 2,150 mwaka 2023/2024.
- Kuongeza idadi ya programu mpya kwa mwaka kutoka programu 1 mwaka 2022/2023 kufikia programu 4 mwaka 2024.

### **Huduma ya Elimu ya Sayansi na Teknolojia**

**53. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kuimarisha elimu ya Sayansi na Teknolojia.

**Matokeo ya muda mfupi;**

- Kuongeza wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi na Teknolojia.
- Kuongeza idadi ya wanafunzi katika fani za ufundi, uhandisi, sayansi na Teknolojia

**Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika fani za ufundi, uhandisi, sayansi na Teknolojia.
- Idadi ya wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi na Teknolojia.

**Shabaha za Utekelezaji;**

- Kuongeza idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika fani za ufundi, uhandisi, sayansi na Teknolojia kutoka wanafunzi 1,880 mwaka 2022/2023 kufikia 2,510 mwaka 2023/2024
- Kuongeza idadi ya wahitimu wa fani za Ufundi, Uhandisi, Sayansi na Teknolojia kutoka 286 mwaka 2022/2023 na kufikia 600 mwaka 2023/2024.

**Huduma ya Mikopo ya Elimu ya Juu**

**54. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wa elimu ya Juu.

**Matokeo ya muda mfupi;**

- Ongezeko la wanafunzi walionufaika na mikopo ya elimu ya juu.
- Ongezeko la wanafunzi wanaorejesha mikopo ya elimu ya juu.
- Ongezeko la fedha zilizorejeshwa kutoka kwa wanafunzi walionufaika na mikopo.

**Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi wanaopokea mikopo.
- Jumla ya fedha za marejesho ya mikopo.

**Shabaha za Utekelezaji;**

- Kuongeza utoaji wa mikopo kwa wanafunzi kutoka wanafunzi 4,875 ya waombaji mwaka 2022/23 hadi kufikia wanafunzi 6,060 ifikapo mwaka 2023/24.
- Kuongeza makusanyo ya marejesho ya mikopo kutoka TSh. 2.9 billion ya mwaka 2022/23 na kufikia TSh. 4.0 billion mwaka 2023/24.

**Huduma ya Uratibu wa Elimu ya Juu**

55. **Mheshimiwa Spika**, Huduma hii ina madhumuni ya usimamizi na tathmini ya elimu ya juu.

**Matokeo ya muda mfupi;**

- Kuimarika kwa mahusiano na mashirikiano mazuri ya uendeshaji wa taasisi za elimu ya juu.
- Ongezeko la wanafunzi wanaopata udhamini wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

**Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo ya elimu ya juu kijinsia.
- Idadi ya wahitimu wa elimu ya juu kijinsia.
- Idadi ya wanafunzi wanaojiunga na vyuo vya elimu ya juu.
- Idadi ya wanafunzi wanaopata udhamini wa kujiunga na vyuo vya elimu ya juu.

**Gharama za Programu:**

Jumla ya TSh. 58,724,112,000/- zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo,

TSh. 31,456,112,000/- ni kwa kazi za kawaida zikiwemo TSh. 22,526,312,000 /- za mishahara ya wafanyakazi, TSh. 8,929,800,000/- kwa matumizi mengineyo na TSh. 27,268,000,000/- kwa kazi za maendeleo.

## **PROGRAMU YA NNE: ELIMU MBADALA NA MAFUNZO YA AMALI**

**56. Mheshimiwa Spika**, Programu hii madhumuni yake ni kutoa elimu ya mafunzo ya amali kwa mwanafuzi kulingana na mahitaji ya soko la ajira. Programu hii ina programu ndogo mbili kama ifuatavyo:

### **Programu ndogo ya Mafunzo ya Amali**

**57. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu itakayowawezesha vijana kujiajiri ili kujikwamua na umasikini.

### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Ongezeko la wahitimu waliopata Mafunzo ya Amali na ufundi na kuweza kujiajiri.

### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya vikundi vya wahitimu wa Mafunzo ya Amali waliopata Mkopo na kujiari.
- Idadi ya wahitimu wa Mafunzo ya Amali.

### **Shabaha za Utekelezaji;**

- Kuongezeka kwa vijana waliojiajiri kutoka vikundi 22 mwaka 2023 hadi kufikia vikundi 34 mwaka 2024.

### **Programu ndogo ya Elimu Mbadala na Watu Wazima**

**58. Mheshimiwa Spika**, Programu hii ina madhumuni ya kupunguza kiwango cha kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu miongoni mwa wanajamii.

**Matokeo ya muda mfupi;**

- Ongezeko la vijana waliorejea masomo baada ya kuacha skuli.
- Ongezeko la watu waliojiunga na madarasa ya wanakisomo.

**Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya vijana wanaojiunga na masomo baada ya kuacha skuli au kutokuandikishwa.
- Idadi ya watu wazima wanaojiunga katika madarasa ya wanakisomo.
- Idadi ya vijana waliojiunga vituo vya elimu ya kujiendeleza.

**Shabaha za Utekelezaji;**

- Kuongeza kiwango cha kujua kusoma na kuandika kutoka asilimia 87.3 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 90 ifikapo mwaka 2025.
- Kuongeza idadi ya vijana waliorejea skuli kutoka 25,961 mwaka 2023 kufikia wanafunzi 35,732 mwaka 2024.

**Gharama za Programu:**

Jumla ya TSh. 37,028,642,302/- zimepangwa kwa ajili ya kufanikisha kazi za programu hii. Kati ya fedha hizo, TSh. 10,044,175,302/- ni kwa kazi za kawaida zikiwemo TSh. 4,133,075,302/- za mishahara ya wafanyakazi, TSh. 5,911,100,000/- kwa matumizi mengineyo na TSh. 26,984,467,000/- kwa kazi za maendeleo.

## **PROGRAMU YA TANO: UBORA WA ELIMU**

**59. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu bora kwa ngazi zote za elimu na programu ndogo tatu na maeneo matano ya kutoa huduma kama yafuatayo:

### **Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Kufundishia**

**60. Mheshimiwa Spika,** Huduma hii ina madhumuni ya kutayarisha mitaala ya elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi za elimu ya maandalizi, msingi, sekondari na mafunzo ya Ualimu.

### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Uwepo wa Mitaala ya Elimu na vifaa vya kufundishia na kujifunzia kwa ngazi zote za elimu.

### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya Mitaala iliyotaarishwa.
- Idadi ya vitabu na vifaa vyengine vya kufundishia vilivyotayarishwa na kusambazwa katika skuli na vyuo vya ualimu.
- Idadi ya walimu walipatiwa mafunzo juu ya mtaala mpya

### **Shabaha za Utekelezaji**

- Kuratibu vikao vinne vya mashirikiano baina ya Taasisi ya Elimu Tanzania na Taasisi ya Elimu ya Zanzibar.
- Kutoa mafunzo kwa walimu wote wa skuli za serikali na binafsi juu ya matumizi ya mtaala mpya wa elimu ya maandalizi na msingi katika madarasa ya maandalizi mwaka wa pili, darasa la pili na darasa la tano.
- Kufanya mapitio ya mitala minne ya mafunzo ya ualimu ambayo ni; Stashahada ya msingi, Stashahada

ya sekondari katika tahasusi ya dini na kiarabu, Astashahada ya elimu ya maandalizi na Astashahada ya elimu mjumuisho.

- Kuchapisha vitabu na viongozi vya mwalimu kwa ngazi ya elimu maandalizi na msingi kwa madarasa ya mwaka wa pili, darasa la pili, darasa la tatu, darasa la tano na darasa la sita.

### **Huduma ya Upimaji na Tathmini ya Elimu**

**61. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kupima na kutathmini utekelezaji wa utoaji wa elimu.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Upimaji wa wanafunzi katika mitihani yao ya taifa.

#### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi na walimu wanaofanya mitihani.
- Asilimia ya ufaulu wa walimu na wanafunzi.

#### **Shabaha za Utekelezaji**

- Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi darasa la nne kuongezeka kutoka asilimia 96.67 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 98 ifikapo mwaka 2023.
- Kiwango cha ufaulu cha wanafunzi darasa la saba kuongezeka kutoka asilimia 86.42 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 88 ifikapo mwaka 2023.
- Kuongezeka Asilimia ya wanafunzi walioandikishwa kufanya mitihani ya kidato cha pili kutoka asilimia 97.29 ya mwaka 2022 na kufikia asilimia 100 mwaka 2023.
- Kiwango cha ufaulu cha mpito kutoka kidato cha pili kwenda cha tatu kuongezeka kutoka asilimia 85.7 mwaka 2022 hadi kufikia asilimia 87 ifikapo mwaka 2023.

## Huduma ya Ukaguzi wa Elimu

**62. Mheshimiwa Spika,** utoaji wa huduma hii una madhumuni ya kusimamia utoaji wa elimu unaofuata mtaala na kuhakikisha ufanisi na ubora wa elimu inayotolewa.

### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Ongezeko la Skuli na walimu waliofanyiwa ukaguzi Viashiria vya matokeo;
- Idadi ya skuli zilizokaguliwa
- Idadi ya walimu waliokaguliwa

### **Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongezeka idadi ya skuli zilizokaguliwa kwa mwaka kutoka skuli 938 mwaka 2022/2023 na kufikia skuli 980 mwaka 2023/24.
- Kuongezeka idadi ya walimu waliokaguliwa kwa mwaka kutoka walimu 2,800 mwaka 2022/2023 na kufikia walimu 2,850 mwaka 2023/24.

## Huduma za Maktaba

**63. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa fursa ya kutumia vitabu na vyanzo vyengine vya taaluma kwa wananchi.

### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Ongezeko la wanafunzi, vijana na wanajamii wanaopatiwa huduma za maktaba.
- Ongezeko la vituo vya huduma za maktaba ili kufikisha huduma kwa jamii.
- Ongezeko la vitabu na vifaa vya kusomea katika maktaba.
- Uwepo wa maktaba mtandao e-library.

### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya watu wanaotumia maktaba.

- Idadi ya vitabu, CDs, vifaa vya elektroniki, magazeti na majarida yaliyopo katika maktaba.
- Idadi ya skuli zenye maktaba kamili.  
Shabaha za Utekelezaji
- Kuongeza idadi ya wanachama waliosajiliwa kwa mwaka kutoka 967 mwaka 2023 hadi kufikia wanachama 1500 mwaka 2024.
- Kuongezeka kwa idadi ya watumiaji wa maktaba kwa mwaka kutoka 44,016 mwaka 2023 hadi kufikia watumiaji 55,000 mwaka 2024.

### **Huduma ya Urajisi wa Elimu**

**64. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuhakikisha Sheria, Sera na taratibu za Wizara zinafuatwa. Pia kutoa leseni kwa walimu na kusajili skuli za Serikali na za binafsi.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Skuli za Serikali na binafsi zenye viwango bora kusajiliwa.
- Leseni za walimu kutolewa.
- Kuondoa matukio ya udhalilishaji kwa wanafunzi.

#### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya leseni za walimu zilizotolewa.
- Idadi ya skuli zilizosajiliwa.
- Idadi ya kesi za udhalilishaji kwa wanafunzi zilizofuatiwa na kutolewa uamuzi.

#### **Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza idadi ya leseni za walimu kwa mwaka kutoka 2,734 mwaka 2022/2023 kufikia leseni 5,554 mwaka 2023/2024.
- Kuongeza idadi ya skuli zilizosajiliwa kutoka 74 mwaka

2022/2023 hadi kufikia skuli 124 mwaka 2023/2024.

- Kuendela kufuatilia kesi zote za udhalilshaji zinazoripotiwa katika Afisi ya Mrajis wa Elimu Unguja na Pemba.

### **Programu ndogo ya Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha**

**65. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kutoa elimu kwa wote wakiwemo watoto wenye mahitaji maalum, kutoa elimu ya stadi za maisha ikijumuisha ushauri na unasihi, jinsia, nidhamu endelevu, madawa ya kulevya na masuala yanayohusiana na afya ya uzazi.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Kuimarika kwa mazingira ya kujifunza na kufundishia kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

#### **Viashiria vya matokeo;**

- Idadi ya wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- Idadi ya skuli zenye mazingira yaliyozingatia mahitaji wa wanafunzi wenye mahitaji maalum.
- Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo ya elimu mahitaji maalum.
- Idadi ya walimu na wanafunzi waliopatiwa elimu za stadi za maisha.

#### **Shabaha za Utekelezaji**

- Kuongeza idadi ya walimu waliosomea fani ya elimu ya mahitaji maalum kutoka walimu 45 kwa mwaka na kufikia walimu 51 mwaka 2023/2024.
- Kufanya ufuatiliaji wa skuli zinazotekeleza utoaji wa elimu mjumuisho kutoka 300 mwaka 2022/2023 kufikia skuli 340 mwaka 2023/2024.
- Kutoa mafunzo ya elimu ya stadi za maisha kwa walimu 186 wa ushauri na unasihi na wanafunzi 41,388 kwa

mwaka 2023/2024.

### **Programu ndogo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA)**

**66. Mheshimiwa Spika,** Programu hii ina madhumuni ya kuifanya teknolojia ya habari na mawasiliano itumike katika kufundisha, kujifunza na katika ngazi ya utawala.

#### **Matokeo ya muda mfupi;**

- Kuimarika kwa matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa elimu.

#### **Viashiria vya utekelezaji;**

- Idadi ya walimu na wanafunzi waliopatiwa mafunzo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
- Idadi ya Skuli zenye vifaa vya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano.
